Nipashe
Alhamisi Januari 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580453
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**TABOA** yataka elimu tiketi za kielektroniki

UKURASA 3



**Sungusungu** mbaroni madai ya wizi fedha za ujenzi madarasa

UKURASA 9


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Shida kubwa watoto wa mitaani Moro na kilio wajengewe makazi

UKURASA 11

# Polisi alivyonaswa tuhuma za uhalifu

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MBUNGE: NINASUBIRI UAMUZI WA CHADEMA**

SIKU mbili baada ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na...

UKURASA WA 4

**JPM KUTETA NA WAZIRI MAMBO YA NJE CHINA**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, anatarajiwa kuwasili nchini...

UKURASA WA 4

**WATUMISHI WADAIWA KUTAFUNA MAKUSANYO**

KATIBU Tawala Mkoa wa Simiyu, Miriam Mmbaga, ametoa muda wa siku...




RPC Arusha Salum Hamduni

# Baba, mama na mtoto wauawa na tembo

UKURASA 3



# Mkuu wa shule akataa rushwa jiwe tanzanite kumbeba mtoto wa kigogo

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA HASIRA KWA NAMUNGO FC UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Mbunge: Ninasubiri uamuzi CHADEMA

**Na Enock Charles**

SIKU mbili baada ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kutoa msimamo kuhusu hatima ya Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Kenan na madiwani 85, mbunge huyo amesema anasubiri uamuzi utakaotolewa na chama hicho.

Juzi, Mbowe alisema hatima ya wabunge 19 wa viti maalum, Kenan na madiwani 85 walioapishwa bila ridhaa ya chama, itajulikana baada ya vikao vya juu vya chama hicho.

"CHADEMA ni taasisi na ina taratibu zake za kufanya uamuzi. Kwa sasa, sina la kusema, ninasubiria uamuzi wa chama," Kenan alisema alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo.

Kwa mujibu wa Mbowe, sakata la mbunge huyo na madiwani 85 nchi nzima kutoka chama hicho walioapishwa kushika nafasi hizo, lina utofauti na wabunge 19 wa viti maalum walioapa kuingia bungeni kwa kuwa hawakutenda jinai kama ambavyo inadaiwa kutendwa na wabunge wenzake ambao wanadaiwa kutokupewa baraka za chama kuapishwa kuwa wabunge.

"Ndugu zangu Watanzania, Mbunge wetu wa Nkasi Kaskazini kutoka Mkoa wa Rukwa na baadhi ya madiwani wameapa na kuingia kwenye vyombo vya kiserikali kinyume cha msimamo wa chama, wengi wanahoji msimamo wa chama.

"Tofauti na wabunge wa viti maalum, mbunge wetu huyu wa Nkasi na madiwani kadhaa hawajatenda jinai bali walikataa kuheshimu msimamo wa chama, chama kitafanyia kazi mazingira ya kila mmoja wao na kuchukua uamuzi stahiki kwa wakati mwafaka," Mbowe alisema.

Tayari wabunge 19 kutoka chama hicho walioapishwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuwa wabunge na kufukuzwa uanachama wa chama hicho, wameshakata rufani katika chama hicho na kupokewa kwa rufani hizo ingawa mpaka sasa haijafahamika ni muda wa kutolewa kwa uamuzi dhidi yao.

# Polisi mbaroni akituhumiwa kunaswa na bangi, gongo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi, amefanya operesheni ya kushtukiza nyumbani kwa mmoja wa askari polisi jijini Arusha na kumkamata akituhumiwa kuiba umeme, kuhifadhi pombe ya viroba zilizopigwa marufuku na serikali.

Vilevile, askari huyo anatuhumiwa kukutwa na misokoto 20 ya bangi ikiwa imehifadhiwa ndani ya pochi, madumu ya mafuta ya petroli, dizeli na gongo yakiwa yamehifadhiwa ndani ya buti la gari lake na baadhi sebuleni kwake.

Akizungumza kwa uchungu, Kigongosi alisema aliamua kufanya operesheni hiyo baada ya kupokea taarifa za kuwapo kwa mtu anayedaiwa kuiba umeme wa Shirika la Umeme (TANESCO) kwa muda mrefu.

"Nilipopata taarifa hii, nilimtaarifu Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha na polisi kisha tukaenda eneo la tukio usiku wa Januari 5 majira ya saa tatu usiku na tulipofika kwenye hiyo nyumba, tukabaini ni ya askari polisi na alikuwapo," alisema.

Kiongozi huyo wa wilaya alisema kitu cha kwanza walikagua umeme wake na kubaini amejiunganishia kienyeji na hajawahi kulipa gharama zozote kwa TANESCO tangu Julai mwaka jana.

"Lakini hili la kutolipa umeme tangu mwaka huo au mwaka mmoja sina hakika, huenda zaidi ya hapo anaiba umeme bila kujali Rais wetu anahangaika kujenga miradi mikubwa ya umeme, wengine wanaiba umeme, tena askari polisi. Hili sikubaliani nalo, niliamuru akamatwe na kuipekua nyumba yake yote," alisema.

Kihongosi alisema kwamba, baada ya kupekua nyumba hiyo, walikuta maboksi mengi ya viroba na chupa za konyagi ambazo anajaza viroba hivyo vilivyopigwa marufuku na serikali.

Alisema askari huyo anatuhumiwa kuzitumia chupa hizo kujaza pombe za viroba na kuwauzia wateja kwenye baa, kitu ambacho ni kinyume cha sheria.

Aliongeza kuwa hawakujua mahali anakotoa mafuta hayo, hivyo wakayahusisha na vitendo vya uhalifu. Alisema kuwa baada ya kumaliza upekuzi ndani ya nyumba hiyo, walipekua ndani ya gari lake na kukuta misokoto ya bangi ikiwa ndani ya pochi imefungwa vizuri na madumu kwenye buti la gari hilo, ambayo askari huyo alidai ni maji na walipomimina walibaini ni gongo na mafuta ya petroli.

Alisema kuhifadhi mafuta ndani ni hatari kwa usalama wa watu wanaoishi humo na hata majirani kwa kuwa kunaweza kutokea mlipuko wa moto.

Alidai kuwa kwenye nyumba hiyo pia walikuta vyuma mbalimbali viinavyodhaniwa kumeibwa kutoka kwenye miundombinu ya serikali.

"Sasa baada ya kumkuta na uchafu wote huu akifanya, nilimkabidhi kwa baadhi ya viongozi wa polisi nilioambatana nao katika operesheni hiyo, ili taratibu zingine za kisheria zifuatwe na afikishwe kwenye vyombo vya kisheria," alisema.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, kuzungumzia hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari huyo, na alijibu kwa kifupi kuwa "askari huyo ni mhalifu kama walivyo wahalifu wengine".



Baadhi ya wanachama wa jukwaa la watoa huduma mkoani Ruvuma linalojumuisha washereheshaji, wapigapicha mbalimbali na wapambaji, waliumaliza mwaka kwa kupeleka mahitaji mbalimbali kwa wahitaji ikiwamo sokoni. **PICHA: MICHAEL EMMANUEL**

# Mkuu wa shule akataa rushwa jiwe tanzanite kumbeba mtoto wa kigogo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Shule ya Sekondari Kisimiri mkoani Arusha, Valentine Tarimo, amedai kukataa kupokea rushwa ya Sh. milioni moja na jiwe la madini ya tanzanite, alilopelekewa ili aruhusu mtoto wa kigogo mmoja kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hiyo mwaka huu. Jana, Tarimo alidai kwa sasa yuko katika majaribu makubwa, akisema mmoja wa wazazi alimfuata na kumpelekea jiwe la tanzanite na wengine wakampelekea fedha.

"Nimekuwa katika majaribu makubwa ya kuletewa rushwa kama juzi kaja mzazi mmoja (hakutaja jina), akaniletea jiwe la tanzanite na wengine wakaniletea fedha Sh. milioni moja au zaidi ya hiyo, ila nimekataa na nitaendelea kukataa. Ninataka watoto wote wenye sifa ya kuja hapa waje bila rushwa," alisema.

Shule hiyo ambayo kwa miaka zaidi ya miaka minne sasa imekuwa iking'ara kwa ufaulu na kuingia 10 bora kitaifa, iko katika Kijiji cha Kisimiri Chini, Kata ya Uwiro, Wilaya ya Arumeru.

Kutokana na jaribu hilo, Tarimo alisisitiza kwamba hatapokea rushwa ya aina yoyote kwa kuwa kufanya hivyo, kutasababisha kunyima fursa watoto wa maskini wasio na kitu cha kuhonga.

Alisema ni vema wazazi wakaacha tabia hiyo ya kushawishi kwa kutoa rushwa, waiache shule ipokee watoto wa hali zote na wasome bila kujali hali zao za kiuchumi.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, kipaumbele cha shule hiyo ni wasichana kutoka familia za jamii za kifugaji, ambao wengi wao hulazimishwa kuolewa ili kukwepa masomo.

"Akija mtoto aliyekumbana na tatizo hili, sisi tunampokea bila kuangalia kigezo chochote, lakini siyo mtu ana fedha zake, eti anataka tumpokee mwanawe kwa sababu ya fedha zake, hilo hapana tena kama aliyeniletea jiwe, hata sikujua la ukubwa gani maana sikutaka hata kuliangalia," alidai.

Alisema wanapopokea watoto wa kike wa jamii ya kifugaji walioopata matatizo ya kutaka kuozeshwa kwa nguvu,wao huwalinda kwa gharama zao zote ili watimize ndoto zao kimasomo.

Alisisitiza kuwa wazazi wasihangaike naye kwa suala la rushwa, ili wapate nafasi shuleni hapo kwa kuwa hatasita na hajawahi kusita kuwajibu kama nafasi hakuna kwa kuwa hajala cha mtu.

Alishauri kwa yeyote anayeona ana fedha, badala ya kupeleka kuhonga kwa walimu, bora akasaidie ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo na siyo vinginevyo.

Alipoulizwa kuhusu kuripoti polisi au Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mwalimu huyo alisema hajawahi kuripoti juu ya kuletewa rushwa ya fedha na jiwe hilo la tanzanite kwa kuwa aliona atakosa ushahidi baada ya kukataa kuvipokea.

"Sikuona haja kwenda polisi au TAKUKURU kwa sababu sikupokea fedha zao wala jiwe nililoletewa ofisini na hivyo nimeona kama ningeenda huko, nisingekuwa na ushahidi wa kuwaonyesha," alisema.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha, James Ruge, aliiambia Nipashe jana kuwa watalifanyia kazi suala hilo kwa kuwa kwa utaratibu wao, chochote wanachokiona kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kinachohusiana na rushwa, lazima kifanyiwe kazi.

HABARI KITAIFA

# Baba, mama mtoto wauawa na tembo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATU watatu ambao ni mume, mke na mtoto, wamepoteza maisha na mwingine kujeruhiwa baada ya kuvamiwa na kushambuliwa na tembo katika kijiji cha Nshabaiguru, Karagwe, Mkoa wa Kagera.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Fred Muhire (45), baba wa familia aliyekuwa akifanya kazi ya kuchunga ng'ombe, mke wake Aneth (33) na mtoto wao Angel mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi sita.

Alisema tukio hilo lilitokea Januari 3, mwaka huu, saa 11:45 jioni wakati mama huyo akienda kisimani kuchota maji akiwa amebeba mtoto mgongoni.

"Mama huyo akiwa njiani, alikutana na kijana mkazi wa kijiji hicho akikimbia na kumwambia anafukuzwa na tembo na kumtaka mama huyo kukimbia. Hata hivyo tembo alikuwa karibu akamfikia na kumshambulia na mwanawe na kuwajeruhi," alisema.

Kamanda Malimi alisema majeruhi hao walipelekwa katika Hospitali ya Nyakahanga kwa matibabu na kwamba walipoteza maisha usiku huo.

"Mume wa mama huyo akiwa katika shughuli zake, alipata taarifa kuwa familia yake imevamiwa na tembo. Alikimbia kwenda kutoa msaada naye akakutana na tembo na kushambuliwa kisha kupoteza maisha papo hapo," alisema.

Malimi alimtaja majeruhi anayeendelea na matibabu katika hospitali hiyo kuwa ni Juma Rashida (18) ambaye anafanya kazi ya kuchunga ng'ombe katika kijiji hicho kilichoko jirani na Hifadhi ya Taifa ya Rumanyika na kuwa hali yake inaendelea vizuri.

Kamanda alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyoko kandokando ya hifadhi, kuchukua tahadhari au kuhama katika maeneo hayo ili kuepuka kukumbwa na madhara kama hayo.

# TABOA yataka elimu tiketi za kielektroniki

**Na Maulid Mmbaga**

OFISA habari wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustafa Mwalongo, amesema elimu ya tiketi za kielektroniki bado ni tatizo kutokana na watoa huduma hizo kuonekana kutokuwa na uelewa wa suala hilo.

Akizungumza na Nipashe katika sendi ya mabasi Ubungo, jijini Dar es Salaam jana, alisema kuna baadhi ya kampuni zimetekeleza agizo hilo, lakini wengine elimu ya tiketi hizo imekuwa kikwazo.

Alisema wanaendelea kuihamasisha mamlaka husika kutoa elimu mpaka Januari 14, wakati huohuo wakiendelea kuangalia kinacho wakwamisha wamiliki wengine kuanza kutumia tiketi hizo.

"Mimi nilitegemea kuwa tarehe 6 Januari ningewaona wataalamu kutoka mamlaka husika wakitoa elimu kwa watoa huduma hapa Ubungo, lakini cha kushangaza hawapo na hata wale waliotengeneza mfumo huo sijaona hata mmoja," alisema.

Alisema mamlaka husika inatakiwa kwenda katika stendi ya mabasi Ubungo kutoa elimu kwa makondakta ili kuwajengea uelewa wa kutumia mashine za tiketi na zianze kwa haraka.

Mmoja wa watoa huduma ya tiketi za kielektroniki Ubungo, Hamisi Maneno, alisema jamii inahitaji elimu zaidi kuhusu suala hilo kwa kuwa uuzaji wa tiketi hizo ni tofauti na wa vitabu.

"Ili elimu iwafikie Watanzania wengi kunatakiwa kuwe na vipindi maalumu vya televisheni vinavyotoa elimu jinsi ya ununuzi wa tiketi hizo ili kurahisisha mchakato huo," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Gilliard Ngewe, alisema wamepokea malalamiko ya changamoto mbalimbali kuhusu tiketi za kielektroniki kutoka kwa wamiliki wa mabasi na wapo katika mchakato wa kuzishughulikia ili kuzipunguza.

"Kwa wale wanaosema kwamba watoa huduma hawana elimu ya kutumia mashine za tiketi sio kweli kwa sababu kuna watu walikaa darasani na kufundishwa jinsi ya kutumia mashine hizo ndio wakakabidhiwa," alisema.

Vile vile, alisema watu waliokabidhiwa mashine hizo ni waliotambulishwa na wamiliki wa mabasi kuwa watasimamia ukataji tiketi katika magari yao, watambuliwa na LATRA na wamesajiliwa na wanaosema hawana elimu inawezekana hawapo kwenye mfumo.

Mmoja wa abiria, Jackline Antoni, alisema ukataji tiketi za mtandao ni mzuri na unawafanya abiria kuwa na uhakika wa safari.

"Zoezi hili pia linamrahisishia abiria kuchagua usafiri anao utaka na kulipia bei inayo tambuliwa kisheria pia linapunguza usumbufu wa kukosa usafiri kwani mwanzo unaweza kutoka nyumbani na kuja stendi halafu unaambiwa gari zote zimejaa," alisema.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA
## KUHUSU UUZAJI WA MAHINDI MEUPE

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Kilimo ulioanzishwa kwa sheria ya Wakala za **Serikali Sura Na. 30 ya mwaka 1997** kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, Wakala huzungusha akiba ya chakula (recycling) kwa kuuza nafaka zilizohifadhiwa ghalani ili kupata nafasi ya kuhifadhi nafaka zingine.

Wakala unatarajia kuuza **tani 33,489.447** za mahindi meupe. Mahindi hayo yatauzwa kupitia kanda zifuatazo za Wakala:-

| NA. | KANDA | KITUO | KIASI KITAKACHOUZWA (TANI) |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Themi | 641.842 |
| 2 | Dodoma | Kizota - Dodoma | 1,295.733 |
| | | Manyoni - Singida | 344.392 |
| 3 | Kipawa | Chang'ombe - Dar es salaam | 393.405 |
| 4 | Makambako | Makambako | 10,427.177 |
| 5 | Songwe | Mbozi - Vwawa | 577.432 |
| 6 | Shinyanga | Shinyanga- (Shinyanga Mjini) | 4,108.813 |
| 7 | Songea | Ruhuwiko - (Songea Mjini) | 4,003.546 |
| 8 | Sumbawanga | Mazwi - (Sumbawanga Mjini) | 9,008.087 |
| | | Laela - (Sumbawanga) | 2,689.020 |
| | **JUMLA** | | **33,489.447** |

i) Mahindi yatauzwa kama yalivyo katika maghala ya Wakala (Ex-Warehouse) yakiwa yamefungashwa kwenye magunia.
ii) Mnunuzi atalipa gharama za ununuzi wa mahindi ndani ya siku 5 za kazi baada ya kupewa idhini ya kufanya malipo na kuchukua mahindi yaliyolipiwa ndani ya muda atakaopangiwa wa kuzingatia kiasi cha mahindi kilicholipiwa.
iii) Mnunuzi atalipia gharama zote za ubebaji na usafirishaji wa mahindi hayo.
iv) Mnunuzi ataonesha bei ya kununulia kwenye barua yake ya maombi pamoja na ghala la kuchukulia.
v) Wakala utapitia, kuchambua na kufanya maamuzi ya bei kwa kuzingatia bei iliyoomba, hali ya soko, gharama za Wakala na Kituo husika cha mauzo.

Hivyo Wakala unakaribisha maombi kutoka Taasisi mbalimbali, wasagishaji, watu binafsi, wafanyabiashara na wadau wa nafaka ili kununua mahindi. Maombi yabainishe bei ya kununulia, kiasi cha mahindi kinachohitajika, ghala la kununulia, anwani ya mwombaji pamoja na mawasiliano ya simu/barua pepe.

Wale wote waliokwisha wasilisha maombi yao katika Ofisi za Wakala kati ya tarehe 30 Disemba, 2020 hadi 5 Januari, 2021 hawatahitajika kuomba tena. Aidha wanunuzi wengine wanatakiwa kuwasilisha maombi mapya kwa kuzingatia maeneo ya mauzo. **Muda wa mwisho wa kupokea maombi umeongezwa kutoka kabla ya tarehe 06 Januari, 2021** iliyobainishwa awali hadi **tarehe 10 Januari, 2021.** Kwa taarifa zaidi mnunuzi anaweza kuwasiliana na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kupitia **Simu namba 026 2963953.**

Maombi yatumwe kwa:

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,
Kizota, Eneo La Viwanda,
S.L.P 1050,
DODOMA.
**Barua pepe:-** info@nfra.go.tz

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

# PM ataka ubora miradi ulingane thamani ya fedha

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametaka miradi inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini lazima isimamiwe vizuri ili kuhakikisha inakuwa na viwango vinavyoendana na thamani ya fedha iliyotolewa na serikali.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana alipozungumza na viongozi wa mkoa wa Ruvuma katika Uwanja wa Ndege wa Songea akiwa njiani kwenda Dar es Salaam baada ya kumaliza ziara yake mkoani humo.

Uwanja huo kwa sasa unakarabatiwa ili kuimarisha huduma za usafiri wa anga mkoani Ruvuma.

Alisema zaidi ya Sh. bilioni 37 zimetumika kuimarisha uwanja huo kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma ikiwamo kuimarisha njia ya kurukia ndege yenye uwezo wa kupokea abiria zaidi ya 150, jengo la abiria na maeneo ya maegesho yenye uwezo wa kuegesha ndege kubwa sita.

Aidha, ukarabati wa uwanja huo utakapokamilika, utaruhusu ndege kutua usiku na mchana.

"Maelekezo ya serikali kwenye maeneo yote muhimu ya miradi isimamiwe kwa kina na hasa thamani ya fedha na viwango vya ujenzi wa miradi yenyewe. Tumeona Sekondari ya Tunduru, majengo ya halmashauri ya wilaya ya Mbinga, barabara ya Mbinga-Mbamba Bay na uwanja wa ndege, utaalamu umetumika na thamani ya fedha ipo," alisema.

Waziri Mkuu aliwataka viongozi hao waendelee kuwahamasisha wananchi kutumia fursa hiyo ya uwapo wa miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa na serikali katika kufanya biashara ili kukuza uchumi wao kwa kuwa wana miundombinu ya kutosha.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwasisitiza viongozi hao wahakikishe wanasimamia matumizi ya miundombinu ya miradi mbalimbali iliyokamilika ili iweze kutumika vizuri zaidi na kwa muda mrefu.

# Watumishi wadaiwa kutafuna makusanyo

**Na Happy Severine,** BARIADI

KATIBU Tawala Mkoa wa Simiyu, Miriam Mmbaga, ametoa muda wa siku saba kwa Mganga Mkuu wa Mkoa kupatiwa majina ya watumishi wa vituo vya kutolea huduma za afya mkoa mzima ambao wanadaiwa kutafuna fedha za makusanyo kwenye vituo vyao.

Mmbaga alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa idara hiyo katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi na Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwenye kikao kazi.

"Mimi sina utani wala urafiki na mtu ambaye ni mbadhirifu wa fedha za umma. Ndani ya siku saba, RMO (Mganga Mkuu wa Mkoa) niletewe majina ya watumishi hao, lakini kwanza wazirejeshe ndani ya muda huo na hatua kali zitafuata dhidi yao," alisema Mmbaga.

Hatua hiyo imekuja baada ya kupewa taarifa na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Hamis Kulemba, juu ya uwapo wa matumizi mabaya ya fedha za makusanyo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Dk. Kulemba alimweleza Mmbaga kuwa wamebaini baadhi ya vituo vya kutolea huduma, makusanyo hayajapelekwa benki na wahusika wakiwauliza wanasema wamezitumia.

"Kuna baadhi ya vituo tumevitembelea, makusanyo yapo, ukiangalia akaunti ni sifuri. Ukiwauliza wanasema wamepeleka kwenye akaunti zao binafsi, wengine wanasema wamezitumia," alisema Dk. Kulemba.

Mganga mkuu aliongeza kuwa katika mkoa huo, kuna tatizo la matumizi mabaya ya mfumo wa utoaji dawa kwa wagonjwa hali ambayo imesababisha vituo vingi kutokuwa na fedha za kutosha.



Waziri Mkuu mstaafu, Joseph Warioba, akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lenye mwili wa mtoto wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, marehemu Rosemary Nyerere, katika Kanisa la Mtakatifu Imakulata, Upanga jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JPM kuteta na Waziri Mambo ya Nje China

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, anatarajiwa kuwasili nchini leo kwa ziara ya kazi ya siku mbili na anatarajiwa kufanya mazungumzo na Rais John Magufuli, Chato mkoani Geita.

Taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa China nchini, ilisema ziara ya waziri huyo ni sehemu ya ziara yake iliyoifanya katika baadhi ya nchi za Afrika tangu Januari 4, mwaka huu.

Kabla ya kuingia nchini, Wang alifanya ziara katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Botswana na Shelisheli.

Ziara ya Waziri Wang inafanyika ikiwa ni wiki chache baada ya mazungumzo ya simu kati ya Rais John Magufuli na Rais Xi Jinping wa nchi hiyo. Pia ni ziara ya kwanza ya Wang nchini Tanzania.

Hivi karibuni, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alisema Rais Magufuli na Wang wanatarajiwa kuzungumzia masuala ya biashara na ushirikiano wa kimataifa.

Pamoja na mambo hayo, Kabudi alitaja masuala mengine yanayotarajiwa kutawala mazungumzo ya viongozi hao kuwa ni uwekezaji katika masuala ya afya, maji, elimu na uzalishaji kutokana na dira ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Tangu mwaka 1991, Afrika imekuwa sehemu ya kwanza kwa mawaziri wa mambo ya nje wa China nje ya nchi kila mwaka. Ziara ya Waziri Wang ni mwendelezo wa ziara kama hizo, ikiwa ni kudumisha na kuendeleza uhusiano mzuri kati ya China na nchi za Afrika, Tanzania ikiwamo," ilisema taarifa ya ubalozi.

"Wakati janga la corona likiendelea, China iko katika harakati za kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo kwa watu kutoka mataifa ya nje pamoja na maambukizi ya ndani. Pamoja na hatua za udhibiti wa ugonjwa huo,

Wang anaendeleza utamaduni huo na amechagua Tanzania kuwa moja ya maeneo ya kutembelea. Huu ni ushahidi tosha wa urafiki wa kweli kati ya China na Afrika," iliongeza taarifa hiyo.

Mazungumzo hayo kati ya Wang na viongozi wa Afrika, pamoja na mambo mengine, yanagusa utekelezaji wa makubaliano ya Mkutano wa Beijing juu ya Ushirikiano wa China na Afrika (FOCAC) na ule wa mshikamano kati ya China na Afrika dhidi ya COVID-19 na mikakati ya kimaendeleo baina ya pande husika.

Pia taarifa hiyo ilisema mazungumzo hayo yatajikita katika ushirikiano katika mapambano dhidi ya corona, ufufuaji uchumi na masuala ya kimataifa na kikanda kwa manufaa ya China na Afrika, Tanzania ikiwamo.

# MATANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF WATER

## REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)

COUNTRY: **Tanzania**

Name of Project: **Second Water Sector Support Project (WSSP II)**
Credit No: **59490**
Project ID No: **P150361**
Assignment Title: **Consultancy Services for Review and Up-Date of the Detailed Engineering Designs and construction Supervision of the Proposed Wastewater Infrastructure for Tanga City**

Tender No.**ME-011/2020-2021/C/18**

Reference No.**TZ-MOW-195742-CS-CQS**

1. This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for the project that appeared in the United Nations Development Business; Issue No. WB5803 – 12/16 of December 21, 2016.
2. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank towards the cost of the Water Sector Support Project (WSSP II) which is part of the Second Water Sector Development Program (WSDP II), and intends to apply part of the proceeds for consulting services.
3. The consulting services (“the services”) include Provision of Consultancy Services for Review and Up-Date of the Detailed Engineering Designs and construction Supervision of the Proposed Wastewater Infrastructure for Tanga City. The assignment includes Review and update of the designs, preparation of the Tender Documents, Supervision of construction of the wastewater treatment plant, sewerage network and sewage pumping stations. The assignment will be undertaken in a period of 30 months exclusive of the Defect Liability Period which will be 12 months.
4. The Ministry of Water (MoW) now invites eligible consultants to express their interest in providing the services. Interested Consultants should provide information indicating that they are qualified to perform the services. The short listing criteria are:(i) core business of the firm and the number of years in business;(ii) experience in similar assignment (Detailed Engineering Design and construction Supervision preferably Water Projects) (iii) experience of having worked in sub-Saharan Africa or similar environment;(iv) technical and managerial capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff. Do not provide CV’s of staff since key experts will not be evaluated at the short-listing stage).Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture or a sub consultancy to enhance their qualifications.
5. The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 1.9 of the World Bank’s Guidelines: Selection and Employment of Consultants [under IBRD Loans and IDA Credits & Grants] by World Bank Borrowers, January 2011, revised July 2014 (“Consultant Guidelines”), setting forth the World Bank’s policy on conflict of interest.
6. A Consulting Firm will be selected in accordance with the Consultant Qualification Selection (CQS) Method set out in the World Bank Guidelines.
7. Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours from 8:00 to 15:30 hours, Monday to Fridays inclusive, except on public holidays.
8. Expression of Interest marked **“EXPRESSION OF INTEREST PROVISION OF CONSULTANCY SERVICES FOR REVIEW AND UP-DATE OF THE DETAILED ENGINEERING DESIGNS AND CONSTRUCTION SUPERVISION OF THE PROPOSED WASTEWATER INFRASTRUCTURE FOR TANGA CITY”** should be delivered in a written form to the address below (in person, or by courier, or by e-mail) by 27th January 2021 at 14:00 hour’s local time.

Physical Address:
The Secretary Ministerial Tender Board
Ministry of Water,
Kolon Building adjacent to DUWASA Head Office, PMU Offices,
Chimwaga Road,
40473 Dodoma, Tanzania

Attention:
Dr. Christopher P. Nditi
Director of Procurement Management Unit
Telephone: **+255 716 308473**
E-mail: pmu@maji.go.tz

**PERMANENT SECRETARY**
**MINISTRY OF WATER**

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF WATER

## REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)

COUNTRY: **Tanzania**

Name of Project: **Second Water Sector Support Project (WSSP II)**
Credit No: **59490**
Project ID No: **P150361**
Assignment Title: **Provision of Consultancy Updating of Environmental and Social Impact Assessment for the Implementation of Water Supply and Sanitation Improvement Projects for Tanga City**

Tender No.**ME-011/2020-2021/C/20**

Reference No. **TZ-MOW-195725-CS-CQS**

1. This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for the project that appeared in the United Nations Development Business; Issue No. WB5803 – 12/16 of December 21, 2016.
2. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank towards the cost of the Water Sector Support Project (WSSP II) which is part of the Second Water Sector Development Program (WSDP II), and intends to apply part of the proceeds for consulting services.
3. The consulting services (“the services”) include Provision of Consultancy Updating of Environmental and Social Impact Assessment for the Implementation of Water Supply and Sanitation Improvement Projects for Tanga City. The assignment is also expected to result into the development of the Environmental and Social Management Plan (ESMP) as well as Health and Safety Management Plan (HSMP) for the implementation of the entailed project activities. The assignment will be undertaken in a period of Ten (10) calendar weeks.
4. The Ministry of Water (MoW) now invites eligible consultants to express their interest in providing the services. Interested Consultants should provide information indicating that they are qualified to perform the services. The short listing criteria are:(i) core business of the firm and the number of years in business;(ii) experience in similar assignment (Environmental and Social Impact Assessment (ESIA)) (iii) experience of having worked in sub-Saharan Africa or similar environment; (iv) technical and managerial capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff. Do not provide CV’s of staff since key experts will not be evaluated at the short-listing stage). Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture or a sub consultancy to enhance their qualifications.
5. The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 1.9 of the World Bank’s Guidelines: Selection and Employment of Consultants [under IBRD Loans and IDA Credits & Grants] by World Bank Borrowers, January 2011, revised July 2014 (“Consultant Guidelines”), setting forth the World Bank’s policy on conflict of interest.
6. A Consulting Firm will be selected in accordance with the Consultant Qualification Selection (CQS) Method set out in the World Bank Guidelines.
7. Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours from 8:00 to 15:30 hours, Monday to Fridays inclusive, except on public holidays.
8. Expression of Interest marked **“EXPRESSION OF INTEREST FOR PROVISION OF CONSULTANCY UPDATING OF ENVIRONMENTAL AND SOCIAL IMPACT ASSESSMENT FOR THE IMPLEMENTATION OF WATER SUPPLY AND SANITATION IMPROVEMENT PROJECTS FOR TANGA CITY”** should be delivered in a written form to the address below (in person, or by courier, or by e-mail) by 27th January 2021 at 14:00 hour’s local time.

Physical Address:
The Secretary Ministerial Tender Board
Ministry of Water,
Kolon Building adjacent to DUWASA Head Office, PMU Offices,
Chimwaga Road,
40473 Dodoma, Tanzania

Attention:
Dr. Christopher P. Nditi
Director of Procurement Management Unit
Telephone: **+255 716 308473**
E-mail: pmu@maji.go.tz

**PERMANENT SECRETARY**
**MINISTRY OF WATER**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole NSSF kwa kulishtukia hili mapema

**KATIKA** toleo letu la jana kulikuwa na taarifa ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kuwaonya baadhi ya waajiri wanaoshirikiana na wafanyakazi wa shirika hilo kulihujumu ikiwamo kutoa rushwa ili kukwepa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao.

Shirika hilo limekemea vitendo hivyo na kuwasisitiza wanachama na wadau wake wanapoona kuna dalili zozote za rushwa wanapotaka huduma katika ofisi zao kuwasiliana na uongozi wa NSSF moja kwa moja na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Mkurugenzi wa Uendeshaji, Mkurugenzi Mkuu au kutoa taarifa hizo kwenye vyombo vya dola.

Tunatoa kongole kwa NSSF kwa kuwaonya baadhi ya waajiri na wafanyakazi wanaotaka kuondoa uaminifu wa wanachama kwa shirika lao linaloegemewa hasa kwa waliostaafu na wanaokaribia kustaafu.

Michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ni tegemeo kubwa la waastafu kwa kuwa ndio pensheni yao ya uzeeni.

Wanachangia mifuko hiyo ili baadaye waweze kuishi bila kuwa msongo wa mawazo ambao wengine huwasababishia kupata magonjwa na kupoteza maisha mapema.

Inapotokea baadhi ya waajiri kushirikiana na baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu wa shirika hilo na waliokosa uadilifu na kuingia katika vitendo vya rushwa kulihujuma ili lisiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, inakosesha imani kwa wanachama wake.

Rais Dk. John Magufuli katika mkutano wake kati ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), watendaji wakuu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Chama cha Waajiri uliofanyika Desemba 28, 2018, Ikulu jijini Dar es Salaam, aliagiza viongozi hao kusikiliza matatizo wanayokumbana nayo wanachama wa mifuko hiyo na wayashughulikie ili kuondoa malalamiko.

Suala kubwa linalolalamikiwa na wanachama ni kucheleweshewa mafao yao wanapokwenda kufuatilia.

Hata hivyo, baadhi ya majibu wanayopewa wanapolalamikia kucheleweshewa mafao ni waajiri kutowasilisha michango kwa wakati kama inavyotakiwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenista Muhagama, katika kutekeleza agizo la Rais Magufuli, mwezi Januari mwaka juzi, alitembelea ofisi za NSSF Ilala, jijini Dar es Salaam na kuzungumza na uongozi wa shirika hilo baada ya kupata malalamiko ya ucheleweshaji wa mafao kutoka kwa wanachama.


Malalamiko hayo yasingesikika kama waajiri wangewasilisha michango kwa wakati na wafanyakazi wa NSSF (baadhi) wangefanya kazi yao kwa uadilifu.

Hata hivyo, NSSF imeendelea kusisitiza kudhibiti mianya ya rushwa kwa kueleza kuwa hivi karibuni katika ofisi ya NSSF Mkoa wa Mwanza, walipata taarifa kutoka vyanzo vyao kwamba, kuna mfanyakazi anatuhumiwa kuomba rushwa kwa mwajiri.

Baada ya kupata taarifa hiyo waliwasilisha kwenye vyombo vya dola na TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) walifanya kazi yao na kufanikiwa kumkamata mfanyakazi huyo ambaye alikuwa ameenda kuchukua rushwa kwa mwajiri.

Kulipa mafao kwa mwanachama aliyetimiza vigezo ni matakwa ya kisheria na shirika hilo limesisitiza mtu ahitaji kutoa rushwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

# Kumeza dawa bila ushauri wa daktari madhara yake ni haya

**MTINDO** wa kufanya uamuzi kujinunulia dawa na kisha kutumia kwa mtazamo binafsi usio na stadi za utabibu, au kupata dawa kutoka kwa asiye na taaluma hiyo, kwa maana bila ya ushauri wa daktari, linazidi kuwa mazoea.

Katika sura ya awali inachukuliwa 'poa' katika jamii, ni mfano wa soka kucheza danadana golini, mbele ya mshambuliaji maarufu 'muuaji wa kimya kimya.'

Wapo baadhi ya waliozoea kujinunulia dawa kwa sababu ya uzoefu wa kipindi kilichopita, kwamba kama aliumwa kichwa akanywa dawa fulani, basi akiumwa tena ataenda kununua dawa hizo hizo.

Anafanya hivyo pasipo kufuata ushauri kwa mtaalamu wa afya na kuanza kutumia au kumpa mwingine kama mtoto, mzazi huyo au mlezi akichukua hadhi ya mjuzi wa utabibu.

Katika kufumbua macho, mtaalamu tunayemuona hata anafikia hatua ya kupewa wadhifa wa kitaaluma kumtibu mgonjwa anakuwa katika mchakato mrefu, darasani hadi mazoezi ya kitaaluma na kuthibitishwa na waliobobea.

Hivyo, mtaalamu huyo daktari hata anapochukua uamuzi wa kumpa dawa fulani mgonjwa, mtaalamu huyo anaangalia vingi katika lengo la kutafuta ukweli na kumsaidia mgonjwa apone.

Inawezekana wanafanya hivyo, kwa sababu hawapendi kwenda hospitali kufanya vipimo na kupata ushauri wa kitaalamu, au kutokana na kuwapo maduka ya dawa katika maeneo yao na urahisi wa upatikanaji dawa hizo.

Wapo waliozoea, pindi wakijisikia hali si sahihi, wanajitosa kununua dawa dukani na kuanza kuzitumia. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kuwa dawa zimetengenezwa ili kutibu maradhi ya namna fulani, baada ya uchunguzi wa kitaalamu na tiba hiyo inafuata utaratibu maalum.

Kwa maana hiyo, mtu anapojisikia vibaya, anatakiwa kwenda kwa mtaalamu wa afya kupata vipimo na ushauri na dawa sahihi kulingana na aina ya ugonjwa au tatizo lilo nalo, baada ya kufanyiwa vipimo na kupewa majibu.

Ikumbukwe, matumizi ya dawa bila kufanyika uchunguzi wa kitaalamu, yanaweza kuwa na madhara makubwa kwenye afya ya mtumiaji, hata kufika janga la kifo, na madhara mengineyo kama kuharibu chembe hai mwilini na kugeuka saratani.

Kwenye suala la kusababisha kifo, inaelezwa na wataalamu wa afya kuwa, dawa ni sumu zinazokabili vimelea vya magonjwa, hivyo kutumia dawa vibaya kunaweza kumfanya mtu akafa.

Si hayo tu, bali wataalamu wa afya wanasema, mtindo wa kununua dawa na kunywa bila kumuona daktari, unaweza kusababisha mtu kuwa na usugu wa maradhi na tatizo la mzio na uraibu wa dawa.

Daktari Mstaafu wa Kituo cha Afya, Sinza Dar es Salaam, Dk. Phoibe Koshuma, anasema kuna mambo mengi ya kuzingatia kabla ya kutumia dawa, ikiwamo umri, kwa kuwa zipo dawa zisizotumiwa na watoto.

Nyingine anataja zina madhara makubwa kwa umri fulani na zipo zisizotumiwa na watoto chini ya miaka 14, nyingine chini ya miaka 12, nyingine hata miaka mitano na kundi la chini ya mwaka mmoja au kundi la chini ya mwezi mmoja.

Anafafanua kwamba, kuna dawa hazitumiwi wakati wote wa ujauzito, zipo zisizotakiwa kutumiwa na mtu mwenye ujauzito wa chini ya miezi mitatu na nyingine hazifai kwa ujauzito wa zaidi ya miezi mitatu. Pia, anabainisha kuwa zipo dawa zinazotibu maradhi fulani, lakini hazipaswi kutumiwa kwa watu wenye maradhi mengine na zipo zinazotibu maradhi ya shinikizo la damu na hazitumiwi na watu wenye pumu.

Vilevile, kuna dawa hazipaswi kutumiwa kwa watu wenye kisukari na nyingine hazipaswi kutumiwa na watu wenye maradhi ya moyo, pia nyingine hazipaswi kutumiwa kwa watu wenye maradhi ya damu.

Katika mtiririko huo, anasema, zipo dawa zinafanya kazi vizuri kabla ya kula, nyingine zinazofanya kazi vizuri baada ya kula, pia zipo zinazotakiwa kutumiwa usiku tu, ili kuleta matokeo mazuri au kudhibiti maradhi mwilini. Zote hizo zinahitaji ushauri.

Nyingine ni ambazo hazipaswi kutumiwa kama tayari mtu ameshatumia dawa nyinginezo na kuna wakati inawezekana kazi za dawa hizo zinafanana au iliyokwishatumiwa na ina nguvu kuliko mpya.

Kwa mujibu wa Dk. Koshuma, watu wasio na taaluma ya afya hawawezi kuzingatia hayo, badala yake wanatumia au kuwapa wagonjwa dawa bila ushauri wa kitaalamu, hivyo suala la kuwaona wataalamu wa afya ni muhimu.

Wale ambao kwa muda mrefu wamekuwa na mtindo wa kutumia dawa, kuwapa watoto au ndugu zao dawa bila ushauri wa kitaalamu, wabadilike na kujali afya zao kwa kutumia dawa kwa usahihi.

## DAWASA yajivunia miradi 22 ya kijamii

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imesema miradi ya kijamii 22 iliyoichukua katika Halmashauri ya Temeke, imesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua tatizo la maji.

Miradi ya kijamii iliyochukuliwa ni Kitunda, Juabile, Kipunguni, Jaika, Korongo Kivule, Juanya Kivule, Mzinga A, Mwanagati, Mzinga B, Matumbi, Keko bora, Keko Mwanga A, Keko Manga B, Machinjioni A, Mbagala Kuu, Kijichi, Serenge, Kingugi, Njia panda ya Mwinyi, Juhudi, Kwa Nyoka, na Mlamayo.

Miradi hiyo kwa asilimia kubwa inatumia visima kama vyanzo vyake vya maji huku ikiwa na uwezo wa kuhudumia wakazi zaidi ya 4,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam jana, Mhandisi wa DAWASA Temeke, Ramadhani Sangali, alisema miradi hiyo ilikuwa chini ya halmashauri na waliichukua mwaka jana kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma hiyo kwa ufanisi.

Alisema kwa kiasi kikubwa miradi hiyo ya kijamii imesaidia kuongeza makusanyo kwa mkoa wa kihuduma DAWASA Temeke na kuongeza mabadilliko ya kiutendaji.

"Miradi hiyo imeondoa malalamiko kutoka kwa wananchi ya ukosefu wa maji kwa kiasi kikubwa," alisema Sangali.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kuboresha huduma ya majisafi kwa kuhakikisha inasimamia utoaji huduma kwa watumiaji maji ya visima binafsi na vya jumuiya kwenye maeneo ambayo mtandao wa maji kutoka Ruvu Juu na Ruvu Chini haujafika.

# Waziri aagiza vigogo RUWASA kutumbuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Anthony Sanga, kutengua uteuzi wa Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Mara, Sadick Chakka, na mwenzake wa Wilaya ya Tarime, Marwa Murasa.

Aweso ameagiza vigogo hao kuondolewa kwenye nafasi zao kwa kile alichokieleza kuwa ni kushindwa kusimamia vyema utekelezaji wa miradi.

Maelekezo hayo aliyatoa jana wilayani hapa alipokagua mradi wa maji wa Magoto ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake mkoani Mara, baada ya kutoridhishwa na utekelezaji wa miradi, ukiwamo mradi huo.

Baada ya kupokea taarifa ya miradi katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Aweso alisisitiza haina uhalisia na kuwaelekeza wataalamu hao kueleza hali halisi ya miradi na si kudanganya.

Awali, Mbunge wa Tarime Vijijini na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mwita Waitara, ambaye aliambatana na Aweso, alieleza adha ya huduma ya maji inayowapata wananchi wake.

Waitara alisema kwamba miradi mingi ya maji wilayani Tarime ina matatizo, hivyo kumwomba Aweso kuchukua hatua kwa wote wanaohusika kuchelewesha utekelezaji wake.

Taarifa ya miradi iliyowasilishwa sambamba na maelezo ya viongozi mbalimbali, ilimchefua Aweso na akalazimika kutofuata ratiba iliyokuwa imepangwa na wataalamu na badala yake aliomba kupelekwa kwenye miradi mingine yenye matatizo ambayo haimo kwenye ratiba.

"Nimepitia taarifa ya wataalamu wetu hapa na hii ratiba waliyopanga sikubaliani nayo. Sasa nataka mnipeleke kwenye miradi mingine na si hii mliojipangia ninyi ili tu kunifurahisha," alisema Aweso.

Baada ya majadiliano ya muda mrefu na meneja wa kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Waziri Aweso, alielekeza msafara alioambatana nao kutembelea mradi wa maji wa Magoto ili kujionea hali halisi ya utekelezwaji wake.

Alipofika kwenye mradi huo na kujionea hali halisi sambamba na kuzungumza na wananchi, Waziri Aweso alisema mradi huo haujatekelezwa kama inavyopaswa.

"Namwelekeza Katibu Mkuu Wizara ya Maji kutengua uteuzi wa mameneja hawa mara moja na wapewe wengine watakaomudu majukumu kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya uhakika na toshelevu," alisema.

Alisema miradi mingi mkoani Mara hairidhishi, hivyo ni muhimu Katibu Mkuu akaitupia jicho RUWASA hususan watendaji wake na kwamba wasiokuwa na uwezo waondolewe na alisisitiza kwamba ni muhimu kujiridhisha uwezo wa wataalamu kabla ya kuwapanga.

Waziri Aweso pia alielekeza miradi yote ya maji iwe shirikishi kwa viongozi na wananchi wa maeneo husika wawe na uelewe wa pamoja wa kinachoendelea ili kuepuka kucheleweshwa ujenzi wake.

Waziri Aweso yuko mkoani Mara kwa ziara ya siku tatu ya kukagua miradi ya maji hususan inayotekelezwa maeneo ya vijijini.




Vyombo vya moto vikipita kwa tahadhari kutokana na barabara kuharibika, njia ya kuelekea Mabibo Sokoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mabula ashangaa mwamko mdogo umiliki ardhi

**Na Munir Shemweta,** LINDI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameshangazwa na mkoa wa Lindi kuwa nyuma katika umilikishaji ardhi.

Kutokana na hali hiyo, ameiagiza ofisi ya ardhi mkoa wa Lindi kutoa elimu kwa wananchi ili waone umuhimu, faida na thamani ya kumiliki ardhi.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi mkoani hapa wakati akigawa hati za ardhi kwa wananchi wa kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo katika Manispaa ya Lindi akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Alisema mkoa wa Lindi uko nyuma kwa wananchi wake kujitokeza kumilikishwa maeneo ya ardhi wànayomiliki na kumbukumbu za mkoa zinaonyesha kuna hati 7,025 zilizotolewa kwa wamiliki wa ardhi. Alisisitiza kuwa idadi hiyo ni ndogo kwa kuwa wananchi wengi hawajaamka na kuona thamani ya kumilikishwa.

"Ofisi ya Ardhi Mkoa mkatoe elimu kwa wananchi umuhimu na faida za kuwa na umiliki wa ardhi. Hapa shida haiko katika kumilikishwa kwa hati za miaka 99 pekee bali hata zile za kimila. Lazima mkatoe elimu hata kwa wale wananchi walio vijijini ili wamilikishwe na kupatiwa hati watakayoitumia kwa faida ya maendeleo," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri aliitaka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Lindi kujipanga na kwenda kwenye maeneo ya kata kuwaelimisha wananchi faida za kuwa na hati ya ardhi kwa kuwa tangu kuanzishwa ofisi hiyo miezi sita iliyopita, ni hati 367 pekee ndizo zilizotolewa, idadi aliyosema ni ndogo ukilinganisha na mikoa mingine.

Aliwaeleza wakazi wa kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo kuwa mkoa huo una maeneo mengi mazuri ya uwekezaji na iwapo watazembea kumilikishwa, kuna hatari wa kayauza kwa bei ya chini kwa kisingizio cha kutopimwa au kuhaulishwa.

"Mkizembea kumilikishwa maeneo yenu sasa na kupatiwa hati, mtu akitaka kuwekeza mtampa kwa bei ya chini kwa kisingizio cha kutopimwa. Mwingine atalichukua na baadaye ataliuza kwa bei kubwa kwa kuwa ulimuuzia likiwa halijapimwa," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wananchi kujitokeza kupima maeneo yao na kuchukua hati huku akisisitiza kuwa hata kama maeneo hayo hawayahitaji, wanaweza kuyapima ili kuongeza thamani na baadaye watakapotaka kuyauza, wafanye hivyo na kupata fedha za kutosha.

Naibu Waziri pia aliwataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuhakikisha wanasimamia ipasavyo makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kwa kuwa fedha hizo ndizo zinazotumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Lindi, Said Kijiji, alimweleza Naibu Waziri kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na ofisi yake kuhakikisha maeneo mengi ya mkoa huo yanapimwa, mwamko wa wananchi ni mdogo.

Alisema ofisi yake ilishatembelea halmashauri za mkoa huo na kuonana na wakurugenzi kwa lengo la kuendesha upimaji na umilikishaji maeneo, lakini Halmashauri ya Mtama pekee ndiyo iliyoonyesha mwamko.

# Kamishna atoa darasa kwa wafugaji nyuki

**Na Christina Mwakangale**

KAMISHNA Msaidizi Ufugaji Nyuki, Hussein Msuya, amewataka wafugaji wa nyuki na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki nchini kujiimarisha kwa kujiunga na vyama vya msingi vya ushirika ili kunufaika na huduma zitolewazo na vyama hivyo.

Msuya aliyasema hayo juzi alipofungua mkutano wa Jukwaa la Ufugaji Nyuki Tanzania (TABEDO) jijini Dodoma.

Msuya alisema kuwa baada ya serikali kufuta kampuni zenye ukomo wa ahadi na yale yasiyo na mtaji ambazo hazikuzi biashara na uwekezaji zilizokuwa zimesajiliwa na BRELA, jukwaa limekutana na wanachama wake kujadili hatima yao.

Pia, Msuya alisema majadiliano hayo yanalenga kuundwa kwa kamati mpya itakayofanya tathmini ya vyama vya msingi vya ushirika wa wafugaji nyuki nchini.

"Hivi sasa hatuelewi hadhi ya vyama vya msingi, hivyo kamati hii itakayokwenda kuundwa leo (juzi), itafanya tathmini kuona ni nini kinaendelea, tukishaelewa sasa tutaenda kuangalia kinachosababisha vyama hivi kusinzia au kufa.

"Kwa kushirikiana na watu wa ushirika, kamati itaangalia ni mambo gani itafanya kuhakikisha vyama hivi vinasimama na kushauri namna bora ya kuunda muunganiko utakaokuwa mbadala wa TABEDO, kuja na mfumo mwingine wa kuunganisha vyama vya ushirika vya msingi," alisema kamishna msaidizi huyo.

Msuya alitoa wito kwa wanachama kutoa ushirikiano kwa kamati itakayoundwa ili kujitendea haki kwa kile alichokisema ni kukata mti na kupanda mti.

Alibainisha dhana ya kukuza viwanda haitatimia ikiwa hakutakuwa na ushirika wa wafugaji nyuki ulio imara, ushirika wa wafugaji nyuki utawezesha kupata nguvu ya kukuza mitaji, kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki, ambayo ni malighafi ya viwanda.

Rudia Issa, Mwenyekiti wa TABEDO, alisema watashirikiana na kamati itakayoundwa ili kuunda vyama vya ushirika vitakavyotoa ufumbuzi wa mahitaji ya wafugaji nyuki nchini.

Alisema kila mfugaji nyuki akitambua umuhimu wa kuwa mwanachama wa ushirika, atanufaika na mafao mbalimbali ikiwamo kupatiwa mikopo kutoka katika taasisi za fedha pamoja na soko la uhakika la mazao yake.

Lemiona Kimeshua ni mfugaji nyuki na mwanachama wa TABEDO, alisema aliacha shughuli za ufugaji nyuki na kubaki kuwa mnunuzi kutokana na kulegalega kwa vyama vya ushirika.

"Baada ya mkazo mkubwa wa serikali kwenye sekta hiyo nimeamua kufufua na kuanzisha mashamba mapya ya nyuki," alisema Kimeshua.


## NOTISI / TANGAZO

**NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART (T) LTD, SUNDI AUCTION MART (T) LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR (T) LTD, BEST GROUP (T) LTD, SALEI AUCTION MART (T) LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/N | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ELISAFI STEPHANO KISIMBO | ELISAFI STEPHANO KISIMBO | FREM ZA BIASHARA | KIBADA- KIGAMBONI | 21/01/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 2. | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | NYUMBA | KIPERA- KISEMVULE - MKURANGA | 27/01/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 3. | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | DAVID ABEL MLAU NA SADIKI NTAHONDI MAPORO | NYUMBA NA SHAMBA | MAJIMATITU – TEMEKE NA MKURANGA | 29/01/2021SAA 04:00 ASUBUHI HADI SAA 06:00 MCHANA<br>02/02/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4. | JUMA NURU MUSHI | JUMA NURU MUSHI | NYUMBA | MBAGALA KUU - TEMEKE | 29/01/2021 SAA 08:00 MCHANA HADI SAA 10:00 JIONI |
| 5. | HUBERT APOLINARY MUSHY | MWANAISHA IBRAHIM HAJI | NYUMBA | MBAGALA KWA KISAUTI - TEMEKE | 05/02/2021 SAA 08:00 MCHANA HADI SAA 10:00 JIONI |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papohapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayo baki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396 /0719922700
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati), akimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mhandisi Mtemi Msafiri (kushoto), baada ya kukagua chanzo cha maji mradi wa Magoto katika ziara mkoani Mara jana. Kulia ni Mbunge wa Tarime Vijijini ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mwita Waitara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Abiria 730 wa treni wakwama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ABIRIA 737 wa treni wamekwama kwa saa kadhaa katika Stesheni ya Dodoma kutokana na njia ya reli eneo la Godegode na Gulwe wilayani Mpwapwa kujaa mchanga kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Hata hivyo, njia ya reli eneo la Kigwe ambalo ilitokea ajali ya treni Januari 2 mwaka huu, imetengamaa na usafiri kurejea kama ilivyokuwa awali.

Mkuu wa Stesheni ya Dodoma, Festo Mugomapayo, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisi kwake, alisema abiria hao 737 wamekwama mkoani Dodoma kwa saa kadhaa kutoka njia ya reli kujaa mchanga katika eneo hilo.

Mugomapayo alisema kutokana na mvua inayoendelea kunyesha, eneo la Godegode na Gulwe hivi sasa halipitiki kutoka na mchanga mwingi kujaa kwenye njia ya reli.

Alibainisha kuwa kutokana na hali hiyo Shirika la Reli (TRC) limeamua kukodi mabasi ya abiria 15, ili kuwasafirisha abiria hao 737 pamoja na wafanyakazi 16 wanaokwenda mikoa ya Pwani.

"Hivi sasa wahandisi wetu wapo eneo la tukio wanaendelea kushugulikia hali hii na tulitarajia kuwa njia ingefunguka saa nne usiku, lakini kutokana na mvua inaweza isiwe hivyo, basi tumeamua kukodi mabasi 15 kwa gharama zetu ili kuwasafirisha abiria hawa waliokwama," alisema.

Akizungumzia kuhusu eneo ambalo ilitokea ajali ya treni na kuua watu watatu, mkuu huyo alisema tayari limeshatengemaa na tayari usafiri umerejea kama ilivyo kuwa awali.

"Katika eneo la Kigwe wilayani Bahi ambako ajali ilitokea na mabehewa sita kupinduka, tayari tumeshapatengeneza na usafiri umerejea na tayari zimeshapita treni mbili za abiria na moja ya mzigo imepita leo (jana)," alifafanua Mugomapayo.

Baadhi ya abiria waliokwama katika safari hiyo, walisema safari yao imekuwa mateso kwao kutokana na treni hiyo kusimama katika vituo kwa muda mrefu.

Mmoja wa abiria hao, Michael John, alisema alitoka mkoani Kigoma Jumatatu saa 12 jioni, lakini treni hiyo imekuwa ikisimama kila kituo kwa muda mrefu na wao kuelezwa kuwa kuna shida.

"Tumetoka tu Kigoma tumefika Uvinza, tukasimama kwa zaidi ya saa moja, tumeenda Tabora tukasimama tena, tunaambiwa behewa moja limeharibika, ikabidi tukae pale kwa saa sita, tumeenda tena Salanda tumesimama kwa saa 12, lakini pale ilipotea ajali tumefanikiwa kupita kwa mwendo mdogo mpaka tunafika hapa," alisimulia John.

Alisema kutoka na kuteseka kwa takribani siku tatu, wanaiomba serikali iwasaidie ili wafike kule wanakokwenda kwa kuwa wameanza kuishiwa fedha za matumizi.

HABARI KITAIFA

## Sungusungu mbaroni tuhuma ubadhirifu fedha ujenzi madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU wa jeshi la jadi Sungusungu katika Kijiji cha Galamba, Kata ya Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, Mahalu Machimu, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kula fedha za wananchi zilizoelekezwa kwenye ujenzi vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kolandoto.

Tukio hilo limetokea juzi kijijini humo wakati Mtendaji wa Kata ya Kolandoto, Mwakaluba Wilson, alipoitisha mkutano wa kijiji kwa ajili ya kuendesha msako kwa viongozi wa Sungusungu wanaodaiwa kutafuna fedha hizo za ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Wilson akizungunza kwenye mkutano huo alisema, amesikitishwa viongozi hao kutafuna fedha za wananchi ambazo zimetokana na michango pamoja na faini zilizoelekezwa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Awali tulipoitisha mkutano wa kijiji wananchi waliazimia fedha ambazo zipo kwenye uongozi wa Sungusungu Sh. milioni 5.8 zitolewe kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa na uongozi ulipohojiwa ukakubali fedha wanazo, lakini kumbe wameshazitafuna," alisema Wilson.

"Tumeitisha mkutano huu wa kijiji ili tuendeshe msako wa kuzipata hizi fedha na baadhi ya viongozi wa sungusungu wamezirejesha na kubaki Sh. milioni 3,5 na wengine wamekimbia, hivyo tumeamua kuondoka na Katibu wa Sungusungu na kumpeleka polisi ili atusaidie mahali fedha zilipo," aliongeza.

Pia, alipiga marufuku uongozi huo wa Sungusungu kutunza fedha za wananchi kwa kugawana kamati na kuagiza ziwekwe kwenye akaunti ya benki ambayo atawafungulia ili kuepuka ubadhilifu huo wa kula fedha za wananchi.

Katibu huyo wa Sungusungu, Mahalu Machimu, alikiri kugawana fedha hizo kwa ajili ya kuzitunza na kuomba apewe muda ili awafuatilie viongozi wengine ambao wamekimbia na kuzirejesha fedha zote, ombi ambalo liligonga mwamba na kupelekwa polisi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alikiri jeshi hilo kumshikilia katibu huyo.

# Gekul 'awashukia' maofisa uvuvi wanaoshirikiana wahalifu

**Na Mbaraka Kambona**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amesema hakuna haja ya kuendelea kuwa na maofisa uvuvi wanaoshirikiana na wahalifu kufanya vitendo vya hujuma wakati kuna vijana wengi wenye nia njema ya kulitumikia taifa wanahangaika na ajira.

Gekul aliyasema hayo alipotembelea kiwanda cha kuchakata samaki Alpha, kilichopo Vingunguti, jijini Dar es Salaam juzi

Kwa mujibu wa Gekul sehemu kubwa ya upungufu wa rasilimali za uvuvi unachangiwa na baadhi ya maofisa uvuvi ambao sio waaminifu wanaoshirikiana na wahalifu kufanya uvuvi usioendelevu unaosababisha kupungua kwa samaki.

"Tulikuwa Kanda ya Ziwa na hapa pia kilio ni hicho hicho malighafi, malighafi zinapungua kwa sababu baadhi ya maofisa uvuvi wanashiriki katika vitendo vya uvuvi haramu, wanashirikiana na wahalifu, hata pale ambapo vyombo vya ulinzi na usalama vinapotaka kufanya operesheni ya kuwakamata wamekuwa wakitoa taarifa kwa wahalifu hao kama ambavyo ilitokea hivi karibuni kule wilayani Babati," alisema Gekul. "Kwanini tuendelee na watu wa namna hii wakati kuna vijana wengi wenye nia njema na taifa lao wapo huko nje hawana ajira na huku ndani ya serikali kuna baadhi ya watu wanahujumu taifa na uchumi wa nchi, hatuna haja kuendelea kuwa na watu kama hawa," alisisitiza Gekul.

Alisema kuwa itakuwa aibu wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza nchini halafu washindwe kuendelea na uzalishaji kwa kukosa malighafi kutokana na kushindwa kudhibiti uvuvi haramu.

Aliongeza kuwa wawekezaji ni muhimu kwa uchumi wa taifa kwa sababu wanalipa kodi na tozo mbalimbali ambazo zinasaidia kukuza pato la taifa, uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa vijana.

Aliwataka maofisa wanaojihusisha na vitendo hivyo kujirekebisha na washirikiane kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama ili kwa pamoja waweze kukomesha vitendo hivyo kunusuru rasilimali za uvuvi.

"Tutimize wajibu wetu tukijuwa kuwa uvuvi haramu ukiendelea tutaviua hivi viwanda na matokeo yake ajira nazo kwa vijana wetu zitapotea," alieleza Gekul.

Aliwataka maofisa uvuvi wote nchini kuendelea kuchukua hatua za haraka kudhibiti hali iliyopo ya upotevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yote yalipo maji na maziwa.

Awali, Meneja wa Uzalishaji wa Kiwanda cha Alpha, Sreejish Srinivasan, akitoa taarifa ya uzalishaji wa kiwanda hicho alieleza kuwa changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni uchache wa malighafi kwa ajili ya kuchakatwa kiwandani hapo na mpaka sasa wanafanya shughuli zao chini ya asilimia 15 ya uwezo wa kiwanda hicho.



Wafanyakazi wa kiwanda cha kuchakata samaki Alpha, wakimwonyesha Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (wa kwanza kulia), minofu ya samaki aina ya pweza ambayo imechakatwa katika kiwanda hicho, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yafikisha wanane mahakamani

**Na Thobias Mwanakatwe**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imewafikisha mahakamani watu wanane kwa nyakati tofauti akiwamo Mhasibu wa Halmashauri ya wilaya na Ofisa Ushirika wakikabiliwa na makosa mbalimbali likiwamo la kughushi nyaraka.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Abdaudi Mbura, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema Desemba 15, mwaka jana, Mhasibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Noeli Kalemela na Katibu wa Afya, Aggrey Nzingana, walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Chunya.

Watuhumiwa hao walifikishwa katika mahakama hiyo wakikabiliwa na kosa la kughushi kinyume na kanuni ya adhabu kifungu cha 337 na 335 pamoja na kosa la matumizi mabaya ya nyaraka za mwajiri kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007 kifungu cha 22. Pia Desemba 22, 2020, Mtendaji wa Kijiji cha Lugombo, Akoya Mwakyonde, alifikishwa mahakamani kwa kosa la kughushi kinyume na kanuni ya adhabu kifungu cha 337 na 335 pamoja na kosa la matumizi mabaya ya nyaraka za mwajiri kinyume na sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007 kifungu cha 22.

Viongozi wa Chama cha Ushirika AMCOS ya Ndandalo, ambao ni Emanuel Mwakajinga, Andy Mwakang' ata, Godbless Mwakajinga na Ofisa Ushirika, Biezeli Elia Malila, walipandishwa kizimba Desemba 23, mwaka jana.

Watuhumiwa hao walikuwa wakikabiliwa na kosa la kughushi kinyume na kanuni ya adhabu 337 na 335 pamoja na kosa la matumizi mabaya ya nyaraka za mwajiri kinyume na sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007 kifungu cha 22.

Aidha, Desemba 28, 2020, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, iliwafikisha mahakamani aliyekuwa Mhasibu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Samweli Mwakyusa na aliyekuwa mganga wa hospitali hiyo, Dk. Philo Nchimbi.

Watuhumiwa hao walifikishwa mahakamani kwa kosa la ubadhilifu wa Sh. 11,185,000 na matumizi mabaya ya nyaraka za mwajiri kinyume na kifungu cha 22 na 28 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Januari 4, mwaka huu, Mwenyekiti wa kitongoji cha Itaja, Nonga Ngangha wa Kijiji cha Bitimanyanga, amefunguliwa kesi mahakamani na TAKUKURU kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

# Madereva wafungiwa leseni kukiuka sheria

Na Thobias Mwanakatwe

MADEREVA 32 wamefungiwa leseni na 299 wamefikishwa mahakamani kutokana na makosa mbalimbali ya usalama barabarani katika kipindi cha kuanzia Desemba 2020 hadi Januari, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Wilbrod Mutafungwa, wakati akizungumza na madereva katika mji wa Tunduma, mpakani mwa Tanzania na Zambia wilayani Momba, mkoani Songwe.

Jeshi hilo limesema miongoni mwa sababu zinazosababisha kutokea kwa ajali nchini ni tabia iliyokithiri ya madereva hususani wa magari makubwa ya mizigo kuendekeza starehe katika vituo wanavyopumzika.

Mutafungwa alisema wamebaini hayo kupitia doria walizofanya barabarani nchi nzima kuanzia Desemba mosi, mwaka jana hadi Januari mosi, mwaka huu.

Alisema katika doria hiyo sababu nyingine zinazosababishwa kutokea kwa ajali hususani magari makubwa ni pamoja na ulevi uliokithiri kwa baadhi ya madereva, wamiliki wa magari kutowathamini madereva wao, kutotengeneza magari na kusababisha kuendeshwa yakiwa mabovu.

Sababu nyingine alizitaja kuwa ni magari yaliyoharibika kuegeshwa pembeni mwa barabarani bila kuweka alama za tahadhari na kuendesha zaidi ya saa 12 bila kupumzika.

Mutafungwa alisema jeshi hilo pia limebaini ukosefu wa mikataba kwa madereva, maslahi mabovu na utumiaji pombe hususani kwa madereva wa magari makubwa ya mizigo kunasababisha kutokea kwa ajali.

Kwa upande wao madereva wa malori walimweleza Mutafungwa kuwa wanapata changamoto nyingi kutoka kwa maaskari na wamiliki wa magari hali inayofanya kazi yao kuwa ngumu.

Naye Mwenyekiti wa usalama barabarani upande wa malori, Angetile Mwakisyala, alisema wamiliki wa malori kuwatesa madereva imekuwa kero kubwa jambo ambalo husababisha wengi kuendesha magari yakiwa mabovu kwa kuhofia kukatwa mshahara wanapopeleka mahitaji yao muhimu.



Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo (kulia), akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto), pamoja na maofisa wa DAWASA alipofanya ziara katika mtambo wa kuzalisha maji Ruvu Juu, Wilaya ya Kibaha Vijijini mkoani Pwani. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Wakurugenzi halmashauri wahimizwa kukusanya mapato

Na Yasmine Protace, MKURANGA

WAKURUGENZI wa halmashauri za miji, wilaya na majiji nchini wametakiwa kupanga mikakati ya ukusanyaji mapato ya ndani kufikia asilimia 50, ili kufanikisha azma ya Rais John Magufuli ya kuwatatulia wananchi matatizo yao.

Naibu Waziri wa TAMISEMI kitengo cha afya, mapato na miundombinu, Dk. Festo Dugange, alisema hayo wakati alipofanya ziara wilayani Mkuranga, mkoani Pwani.

Dugange alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mkuranga, Mhandisi Mshamu Munde, kwa kukusanya asilimia 42 ya mapato kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, mwaka jana.

"Kwa sasa halmashauri zote zinatakiwa kutimiza malengo ya ukusanyaji mapato, nampongeza Munde kwa kufanikiwa kukusanya mapato kwa asilimia 42 kutoka Januari hadi Novemba, mwaka Jana, mwezi Desema mapato ya makusanyo bado hayajaingizwa taarifa zake," alisema.

Pia, alimtaka Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkuranga, Stephen Mwandambo, kusimamia uungaji wa mifumo ya TEHAMA kwenye zahanati na vituo vya afya ili kuboresha mapato ya sekta hiyo.

Alimtaka kuhakikisha maboresho yanafanyika katika Mfuko ya Afya ya Jamii (CHF) kwa kuhakikisha pesa zinaingizwa katika akaunti na hatimaye wanufaika wapate kadi na pesa ziboreshe huduma za afya.

# DC Kibaha akagua shule za sekondari

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo, amefanya ziara kukagua maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule za sekondari za wilaya hiyo.

Ntemo alifanya ziara hiyo jana kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani la kuhakikisha wanafunzi waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza wote wanaanza masomo Januari 11.

Akiwa katika shule hizo, Mkuu huyo wa wilaya alikagua vyumba vya madarasa, vyoo pamoja na madawati na shule nyingi zilikutwa na maandalizi ambayo yatawawezesha wanafunzi wote kupokelewa.

Pia, alitoa agizo kwa shule za sekondari ambazo zinakwama kutatua vikwazo, kujifunza kwa walimu wakuu wengine ili kuwa na shule ambazo mazingira yake yatawavutia wanafunzi kukaa shuleni.

"Kila shule niliyopita nimejionea ambao hawajakamilisha wapo kwenye hatua za mwisho, niwaombe wale ambao kuna sehemu wanakwama watembelee shule zilizofanya vizuri zaidi katika ujenzi wa vyumba vya madarasa na madawati wajifunze kwao ili isiwepo shule ambayo hali yake hairidhishi," alisisitiza Ndemo.

Ntemo alisema ziara hiyo ni ya awali na wanafunzi watakapofungua shule atatembelea tena shule hizo na kujionea wanavyokaa darasani.

Aliwataka walimu na wazazi kuona ni wajibu wao kila mmoja kuhakikisha wanafunzi wanapata sehemu za kukaa wakiwa shuleni.

Katibu Tawala Wilaya ya Kibaha, Sozi Ngate, aliwatahadharisha wakuu wa shule suala la michango kwa wazazi hususani ya vyumba vya madarasa na madawati.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa Kibaha, Jenifa Omolo, alisema kila kiongozi anatakiwa kusimama katika nafasi yake kujadiliana na wananchi wake namna ya kutatua vikwazo katika sekta ya elimu badala ya kusubiri serikali pekee.

Omolo alisema serikali itaendelea kutoa fedha kumalizia maboma ya majengo ya madarasa ambayo hatajakamilika ili kuondoa uhaba wa vyumba vya madarasa shuleni.




Naibu Waziri alipotia nyayo kukagua afya inavyoendana na kasi Mkuranga

Ukurasa 12



Ukurasa 13

Usafi wa hedhi shuleni waiumiza kichwa Manispaa Bukoba kutatua



Ukurasa 14

Utafiti unaosaka kilichojificha ndani ya Covid –19 unavyoibua mapya yake

# Shida kubwa watoto wa mitaani Moro na kilio wajengewe makazi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KUNA kilio ndani ya Manispaa ya Morogoro, watoto wasio na makazi wanaotangatanga mitaani wanaumizwa katika namna ya kudhalilishwa na hata kuathiriwa kiafya.

Ni kilio kinachoenda mbali, hata kufikia adha ya baadhi ya watu katika umma wasio na mapenzi nao wanawalawiti na kuwabaka.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Amisa Kagambo, bali na kukiri kujua adha hiyo, anasema hatua ambayo mamlaka ya kiserikali Manispaa ya Morogoro inafanya, ni pamoja na kuwakusanya watoto hao kutoka mitaani.

Amisa anasema, baada ya kuwakusanya huwa wanawapeleka kwenye makao saba maalum yaliyopo ndani ya manispaa, akizitaja kwa baadhi yao ni pamoja Fungafunga, Raya, Mission to the Homeless, Mehayo, Agape, Mgolole na Darul Muslim

Hata hivyo, Ofisa Ustawi Jamii huyo, anasema ambao katika sura ya pili inaangukia shida, baadhi ya watoto mara baada ya kuwakamata kwenye matukio mbalimbali, huwa baadhi wanatoroka na kurejea mitaani.

Anasema wanapowapata watoto hao mitaani, kabla ya kuwapeleka kwenye kambi huwatafuta wazazi wao na kuzungumza nao kuhusu malezi yao, kutokana na sheria inavyowataka wazazi kuwalea wao wenyewe na sio kuwaacha wakidhurura mitaani.

Ofisa Ustawi Jamii anasema, wapo wazazi wanaokubali kuwachukua na kwenda kuwalea na wengine huwakataa kwa madai ya kukerwa na tabia mbaya wanazokuwa nazo watoto wao, hata baadhi wanalazimika kuwafikisha mahakamani.

Anasimulia chanzo cha watoto hao kuingia mitaani, ni kwamba wapo wenye wazazi wote wawili, pia kuna mazingira mzazi mmoja au wote wawili kufariki, ikiwamo maradhi ya Ukimwi.

Kuna malalamiko kutoka Ofisa Ustawi wa Jamii, kwamba kuna watoto wenye ujeuri uliopitiliza wao wanaowakera kufikia hatua ya kuwakataa na kinachotawala baada ya hapo kutoelewana na wazazi.

Hapo ndipo kunakuja dhana watoto kukosa chakula na wazazi kuwa na vipigo visivyohesabika kwa watoto, na ndio mwanzo wa safari ya mtoto kuhamia mitaani.

**WAKAZI**

Flora Msangi, mkazi wa Manispaa ya Morogoro, anasema ujenzi wa nyumba au kituo maalum cha kukaa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, unasaidia kupunguza idadi kubwa ya wale wanaoonekana kwa wingi mitaani kwa sasa.

Anatoa hesabu kwamba, kila siku huwa anawaona watoto wa mitaani watano hadi sita na kuna



Baadhi ya watoto wa mitaani wa mjini Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

wakati anawaona wakiwa kundi kubwa mitaani mjini Morogoro, japo linalomtia shaka kubwa.

Florah anarejea kumbukumbu wakiwa kwenye majukumu yao ya biashara kwenye Mtaa wa Kitope katikati ya Manispaa Morogoro, walimwokota mvulana katika eneo la jirani na Mto Morogoro, mwenye umri wa kati ya miaka nane na tisa, akiwa hajitambui.

Anasimulia walimfikisha mtoto huyo Polisi na kisha akapelekwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro kwa matibabu.

Mama huyo anasimulia kwamba, baada ya matibabu mtoto aliamka na kuelekeza kwao kwa kuogopa ni eneo la Mwembesongo na walijaribu kupatafuta pasipo mafanikio.

Anasema walitumia mbinu ya kumbembeleza, baadaye akapataja kwao na walipopatafuta walipapata na baada ya mtoto kupona walimpeleka kumkabidhi kwa mama yake.

Florah anasema, watoto wa aina hiyo wamekuwa wakiingia mitaani katika maisha ya kuomba na kuishia kubakwa au kulawitiwa na watu waliokosa staha na ubinadamu, wakiwapa vitu vidogo vya kuwashawishi.

Mama huyo ana mtazamo kwamba watoto wengi wamekuwa wakizunguka mitaani kuomba, akihisi huenda ni sababu ya kipato kidogo cha wazazi au hali mbaya kwa jumla nyumbani.

Anahimiza suala la kujenga kituo kwa ajili yao sambamba na serikali kuweka sera na kusimamia sheria za haki za mtoto zilizopo, itasaidia wazazi wengi kujua wajibu wao katika kuwatunza watoto wao.

AFYA

# Naibu Waziri alipotia nyayo kukagua afya Mkuranga inavyoendana na kasi

## • Hospitali kuu taabani, bima afya nayo • Mbunge Ulega aja upya akifunguka




Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) anayeshughulika na Afya na Miundombinu, Dk. Festo John, alipotembelea duka la dawa lililopo katika Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

USIMAMIZI wa miradi ya maendeleo sehemu husika inachangia kukua kwa maendeleo, mojawapo ikiwa ni vituo vya afya, lengo ni kuiona inakuwa na sura ya faida kwa umma.

Tayari kuna maelekezo kwa waganga wafawidhi katika vituo vya afya nchini, wanatakiwa kusimamia vyanzo vyao vya mapato katika maeneo ya kazi, lengo ni kuhakikisha huduma za afya zinazidi kuboreshwa.

Dk. Festo John Diganga, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI) anayeshughulikia afya na miundombinu, ametoa maelekezo kutaka wahusika wote kuwa na usimamizi bora wa vyanzo vya mapato vilivyoko.

"Kila vituo vya afya vihakikishe vinasimamia vyanzo vya mapato ili kusaidia kuwapo na upatikanaji wa huduma bora za kiafya," anasema, katika ziara maalum wiki hii wilayani Mkuranga, kukagua huduma za afya na miundombinu.

Dk. Diganga anatoa maelekezo kwamba, vyanzo vya mapato vinapaswa kusimamiwa, hali itakayosaidia kufuata mwongozo unaotaka asilimia 67 ya kipato hicho kiangukie kununua dawa.

Anasema, iwapo kila kituo kitajipanga kusimamia vyanzo vya mapato itawasaidia kununua vifaa tiba na kupewa dawa kutoka shirika la dawa - MSD.

Naibu Waziri anasema vituo vya dawa vikisimamia vizuri, vyanzo vya mapato kitaifa vitaacha kuwa tegemezi au kuwa visimamizi katika mapato ya kununua itawasaidia kununua vifungashi.

> **"Hospitali kwa siku inatakiwa kuhudumia watu 80, lakini kwa sasa inahudumia wagonjwa 300 kwa siku, ambayo ni sawa na asilimia 375 ya uwezo wake.**



Dk. Festo John (katikati),akizungumza na mtumishi wa Hospitali ya Wilaya Mkuranga, kuona anavyofanya kazi ya kutumia mfumo wa kisasa kuchukua takwimu za wagonjwa hospitalini.

Anaongeza kuwa mifuko ya bima, inapaswa kusimamiwa vizuri ili wananchi wawe na imani nayo na anafafanua:"Wapo watu wasio waaminifu ambao wanachukua pesa za wanachama na kushindwa kuzipeleka pesa benki kwa wakati na hali hiyo inachangia kuleta usumbufu."

### TAARIFA WILAYA MKURANGA

Anasema katika taarifa za afya aliyopewa Mkuranga, alibaini kuwapo kasoro zinazotakiwa kufanyiwa kazi na anasema kwa kipindi cha miezi sitailipa Mkuranga malipo yao, lakini cha kushangaza hakuna hatua zilizochukuliwa.

Naibu Waziri anaongeza kuwa huduma duni zinatolewa kwa wagonjwa wenye kadi za CHF zimekuwa na malalamiko kutoka kwa wagonjwa wanaodai hata baadhi ya dawa na vipimo, wanaambiwa hazipo. Mkazo wake ni kwamba, kinachotakiwa ni jamii kuelimishwa juu ya mifuko hiyo, ili waweze kujiunga na kunufaika nayo.

Pia Naibu Waziri huyo, anauagiza uongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga kusimamia vyanzo vya mapato ili kuleta maendeleo.

Bosi huyo mwandamizi kutoka TAMISEMI anautaka uongozi wa Wilaya Mkuranga, kuhakikisha mwezi uliopo wanakifungua Kituo cha Afya Mkuranga, ili kuwapunguzia kero wananchi wanaohangaika kupata huduma hiyo.

"Hii zahanati ni nzuri, nimeitembelea na nimeiona. Kinachotakiwa ni mwishoni mwa mwezi huu kufunguliwa, ili wananchi waanze kunufaika na huduma za afya," anasema.

Mkuu wa Wilaya Mkuranga, Filbeto Sanga, kupitia mkutano huo, anasema pamoja na watu kujiunga katika mifuko bima ya jamii, bado kuna malalamiko ya upatikanaji dawa, akiwa na ufafanuzi:

"Unakuta mtu anayo kadi, anapofika kupata matibabu, anaambulia dawa aina moja wakati ameandikiwa dawa aina mbalimbali."

Anafafanua kwamba kuna changamoto nyingine ya vipimo kukosekana wagonjwa wanapoenda kwenye vituo vya afya vya binafsi, wanakuta kuna dawa nyingi, upungufu ambao Mkuu wa Wilaya anasema, unapaswa kufanyiwa kazi.

Pia, Sanga ansema wazee wanapofika kwenye vituo vya afya vya serikali, nao wanaangukia shida hiyo ya kutakiwa kupatiwa majibu waache kulalamika.

Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega, ambaye alishawahi kuwa naibu waziri katika awamu iliyopita ya serikali, anasema huduma za afya za watu wengi kujiunga ni shida kutokana na wengi hawavutiwi nalo, jambo ambalo wataalamu husika wanatakiwa kuliangalia.

Anarejea uhalisia kwamba, kuna wakati watu wanafika katika mikasa hiyo wakiwa na kadi zao, badala ya kupata matibabu na dawa wanaambiwa hakuna dawa na kipimo.

Pia, Ulega katika mkutano huo anaipongeza serikali kwa hatua ya kuwawezesha fedha za kuongeza ufanisi katika hospitali hiyo ya wilaya, kwani hadi sasa hospital hiyo imeelemewa kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa.

Anasema hospitali kwa siku inatakiwa kuhudumia watu 80, lakini kwa sasa inahudumia wagonjwa 300 kwa siku, ambayo ni sawa na asilimia 375 ya uwezo wake.

Ullega anabainisha baadhi ya huduma kama za wazazi kujifungua ni za bure, ambazo ni kwa mujibu wa sera za kitaifa, hapo ikijumuisha 'x-ray' na 'ultrasound.'

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga, Steph Mbwambo, anatoa taarifa ya mwaka mmoja ya afya katika wilaya hiyo, akisema hivi sasa wanadhibiti mapato kutokana na kufunga vifaa vya kisasa.

Anasema wanahitajika wafamasia watatu, lakini hakuna hata mmoja; wauguzi waliopo ni 86 badala ya 228; wataalamu dawa ya usingizi ni watano, badala ya 12.

Wakati hadi sasa kuna jumla ya vituo 42 vinavyotoa chanjo za binadamu, analalamika kuna shida magari manne ya kubeba wagonjwa ni mabovu.

Mganga Mkuu anakiri, tatizo la kujiunga na Bima ya Afya bado haliridhishi, ingawaje kuna hatua iliyopigwa kutoka wanachama 812 na sasa wapo 2,462.

AFYA

# Usafi wa hedhi shuleni waiumiza kichwa Manispaa Bukoba kutatua

• Maji, vifaa, miundombinu haiko vizuri

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

KUNA kilio cha hedhi kumnyanyasa mtoto wa kike wa shule ya msingi ndani ya Manispaa wa Bukoba, Mkoa wa Kagera wanapoteza vipindi vya masomo hadi 137 kwa mwaka, sawa na wiki 19 hadi 20.

Ni kelele zinazowaamsha wadau kushirikiana na serikali, wanafanya jitihada kuhakikisha shule inakuwa katika mazingira salama kwa mabinti masomoni.

Hapo kunajengwa vyumba maalumu vya kuwahudumia usafi na kubadilisha vifaa vya hedhi na kuna waraka wa elimu unaozitaka shule kuwanunulia mabinti vifaa hivyo, hasa wanaoingia hedhi ghafla masomoni. Ni jitihada zinazokabiliana na kasoro ya baadhi ya shule kutokuwa na vyumba vya faragha na maji ya uhakika, ambavyo ni hitaji muhimu kwao.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Tumaini, wakiwa katika mkusanyiko wa kishule Manispaa ya Bukoba. **PICHA: MTANDAO**

### OFISA ELIMU

Florence Kibani, Ofisa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, anayeshughulika na Afya, Lishe na Usafi wa Mazingira katika shule za msingi na sekondari za Bukoba, anataja mwaka wa masomo una siku 194 za darasani.

Mwongozo wa serikali unafahamisha, kila mwaka wa masomo una mihula miwili, kila moja na wiki 21.

Kibani anasema panapokuwapo mazingira ya shule sio salama kwa binti, maana yake anapoingia hedhi, inakuwa kikwazo kwake kwenda shule. Anafafanua: "Ukichukua siku nne anazopoteza kila mwezi, ukazidisha mara miezi kumi, mtoto wa kike anaweza kupoteza wastani wa siku 40 bila kwenda shule kwa mwaka mzima."

Ofisa huyo anaeleza mtoto anaposhindwa kwenda shule kwa siku 40, anapoteza wastani wa vipindi 137 kila mwaka, hali inayochangia kurudi nyuma kitaaluma.

Ili kuhakikisha mazingira ya binti shuleni yanakuwa salama, kila shule inapaswa kuwa na maji ya uhakika, chumba cha faragha kwa msichana anapoingia kwenye hedhi shuleni, masuala anayotaja bado hayatekelezwi vilivyo.

Anasema, Manispaa Bukoba ina shule za msingi 47, kati yake 25 za serikali 25 na binafsi 22, akiitaja mojawapo ya Rwemishasha isiyo na huduma ya maji, kutokana na tangi pekee lililotegemewa kuharibika.

Kibani ana ufafanuzi kuwa shule saba za msingi za serikali hazina maji ya uhakika, kwa sababu ya kutegemea maji ya matangi yanayovunwa kutoka mvua, ambayo hayatoshelezi mahitaji. Anasema ni hali inayowalazimu wanaosoma katika shule hizo kuchota maji mtoni kwa ajili ya matumizi mbalimbali, ikiwamo chooni.

> **Ukichukua siku nne anazopoteza kila mwezi, ukazidisha mara miezi kumi, mtoto wa kike anaweza kupoteza wastani wa siku 40 bila kwenda shule kwa mwaka mzima.**

Shule za msingi zinazokosa maji ya uhakika anazitaja kuwa ni Kyakailabwa, yenye wanafunzi 1,072, wakiwamo 39 wa Mpango wa Elimu Maalumu kwa Walioikosa (MEMKWA). Anasema shule hiyo ina tangi moja la maji lenye ujazo wa lita 5,000 inayotegemewa kwa mahitaji mbalimbali, ikiwamo kupika uji na matumizi ya chooni, katika makadirio ya mgawanyo wa wastani lita 4.6 kwa kila mtoto.

Kibani anasema, ili kuwapunguzia watoto adha ya kutembea kilomita nne kwenda kuchota maji mtoni, shule inahitaji matangi yenye ujazo angalau lita 12,000.

Anasema, mwaka 2016 lilipotokea tetemeko la ardhi Bukoba, vyoo vya shule hiyo vilididimia na muda mfupi baadaye Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef), liliwanusuru kwa kujenga vyoo vipya, pia kuweka chumba maalumu kwa mabinti kujisitiri wakati wa hedhi.

Anasema, Shule ya Msingi Kyakailabwa kwa sasa ina watoto kuanzia darasa la tano hadi la saba na kati yao waliokwishaanza hedhi wako 83. Ana ufafanuzi: "Kwa sababu wote hawaingii kwa wakati mmoja, chumba hicho kinawasaidia.

"UNICEF pia, ilijenga vyoo na kuweka vyumba maalumu vya watoto wa kike katika shule nyingine saba za msingi ambazo ni Ihungo, Mugeza Mseto, Nyamukazi, Mafumbo, Bilele, Kibeta na Kitendaguro."

Ofisa Elimu huyo, anaeleza walivyojenga sehemu ya kutupa taka za hedhi katika shule sita na wakaweka sehemu maalumu ya kuchoma taka. Katika shule mbili, uchimbaji mashimo ulishindikana kutokana na ardhi yake kuwa na maji mengi.

Anasema vyoo vingine vilijengwa na Shirika la World Vision Tanzania, katika shule nne, kila shule zikiwa na jumla ya matundu manane.

### KUPATIKANA TAULO

Kuhusu upatikanaji taulo za kike, Kibani anasema wamekuwa wajitokeza wafadhili, akiwawataja baadhi ni mashirika ya Orthodox na Jambo Bukoba, wanaotoa vifaa vya kujisitiri kwa baadhi ya shule za msingi, akizitaja: Kyakailabwa, Mafumbo na Bugambakamoi.

Anafafanua kuwa, watoto wanapoingia kwenye hedhi wakiwa nyumbani wanahimizwa kwenda shuleni na vifaa vyao, vikijumuisha vinavyonunuliwa chini ya Waraka wa Elimu Namba Sita wa Mwaka 2015 na vinavyotolewa na wafadhili, vyote kutumiwa na watoto walioingia hedhi ghafla shuleni.

### MADHARA JE?

Kuhusu madhara yanayoweza kumpata mtoto asiyepata majisafi ya kujisafisha na kubadilisha vifaa vya hedhi, anataja ni kukumbwa na magonjwa kama muwasho na upele katika sehemu za siri.

Hatari nyingine ni msichana kupata saratani ya mlango wa kizazi (HPV), kwa sababu kifaa anachotumia kuna wakati anakosa sehemu maalumu ya kubadilishia, pia kujisafisha.

"Mtoto analazimika kukibeba kwenye mfuko, kinahifadhiwa katika mazingira yasiyo salama, akija kukirudia inawezekana kikawa na 'kutu' kikamletea madhara kwenye viungo vyake vya uzazi," anasema.

Mengine anayotaja ni harufu mbaya inayosababishwa na kukaa na vifaa muda mrefu, hata wenziwe hasa wa kiume wanaanza kumnyanyapaa na kumtenga.

Kibani anadokeza kasoro ya mtoto kuumia kisakolojia akikosa kujiamini darasani na hata inatokea anatakiwa kusimama kujibu swali, anashindwa kutokana na hofu ya kuumbuka.

Hivyo, anatoa wito kwa wazazi na walezi kuwajibika na gharama za matumizi ya kununulia mtoto vifaa vya hedhi, jamii nayo iingilie kati kwa misaada wa kuwawezesha kuhudhuria siku zote za masomo.

### WANAFUNZI WALIKOSIMAMA

Jackline Kokwenda (sio jina lake halisi), mwanafunzi aliyeko darasa la MEMKWA katika Shule ya Kyakailabwa, anasema shule yao ina tangi la kuvuna maji ya mvua, lakini kila siku wanaenda mtoni kuchota maji ya kupikia uji, kutumia choonii na kusafisha vyumba vya madarasa.

Mwanafunzi huyo mwenye umri miaka 15, anasema, tangu alivyoanza kuingia kwenye hedhi, lakini hajawahi kubadilisha vifaa vyake akiwa shuleni.

"Nikiingia kwenye hedhi nakaa siku nne na ninapokwenda shuleni sibadilishi mpaka nirudi nyumbani," anasema.

Anasema, huwa anazikatisha kwa kuzifua na namna ya kujihifadhi shuleni, alifundishwa na dada yake.

Pia, anasema hajawahi kupewa kifaa cha kumsaidia akiwa kwenye hedhi shuleni, lakini ameshuhudia wenzake wakipewa na walimu wanapoingia hali hiyo shuleni.

### MZAZI NA YAKE

Zobia Tibawa, mzazi mwenye binti wa wa umri wa kuingia kwenye hedhi, anasema wazazi wanalazimika kuwafundisha watoto namna ya kujihifadhi, hata wakawa salama shuleni, kwa vifaa rasmi.

Mama huyo anasema alimfundisha mwanawe kutumia mbadala kwa sababu ya kukosa uwezo wa kununua vifaa hivyo kila mwezi.

"Unamwelekeza namna ya kukitumia, lakini unamfundisha namna ya kukifua na kukianika, ili kiweze kutumika wakati mwingine," anasema.

Anasema ni somo linaloendana na stadi za kukwepa uhusiano wa kimapenzi na wanaume unaozaa mimba, hata kuwakatisha masomo.

"Kwa sasa watoto wanaingia kwenye hedhi wakiwa wadogo, unakuta mtoto wa darasa la tano tayari kaingia! Ni tofauti na sisi zamani tulimaliza hadi darasa la saba bila kuingia.

"Inawezekana hata vyakula wanavyokula watoto siku hizi, vinachangia maana zamani tulikula zaidi vyakula vya asili," anasema.

AFYA

# Utafiti unaosaka kilichojificha ndani ya Covid –19 unavyoibua mapya



Watafiti wa kimataifa, wakisaka majibu ya usugu wa corona na namna ya kuikabili. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

MENGI zaidi yameanza kueleweka na kuthibitishwa na mashirika tofauti ya kimataifa pamoja na wataalamu wa utafiti wa virusi, kuhusu chanzo halisi cha virusi vya corona, vilivyoibuka kuelekea mwisho wa 2018 katikati ya Jimbo la Hubei nchini China.

Ni utafiti unaolenga mabadiliko kutoka virusi vya kawaida vya homa ya mafua vilivyokuwapo tangu 2012 na havikupata chanjo, ila kubadilika kwake kuwa Covid-19 (inayoitwa SARS-2 kitaaluma) ndiko kuliibua shaka.

Watafiti walitaka kujua ni katika hatua gani ya kupita kutoka mnyama hadi binadamu 'virusi hivyo vilibadilika, hasa kwa kufuatilia mgonjwa wa kwanza ('patient zero' kitaaluma) aliingiwa na virusi vya aina gani, vya mnyama au la.

Mwandishi mmoja mwenye uzoefu wa masuala ya upekuzi na msomi wa ngazi ya uzamivu, aliandika katika jarida la utafiti amani la Taasisi ya Usalama wa Kimataifa ya Begin-Sadat nchini Israel, anasema katika mada iliyochapishwa katikati ya mwezi wa Desemba 2020 kuwa kuna mabadiliko katika fikra ya wanataaluma kuhusu chanzo cha mfumo wa virusi vya Covid-19.

Anasema, licha ya chanzo cha kutoka mnyama hadi binadamu hakijaondolewa mezani kama eneo la utafiti, kielelezo kinachoingia akilini zaidi ni kufumuka kwa maambukizi kutokana na vyanzo ambavyo si vya kimaumbile. Ila watafiti hao wanasema inaonekana mfumuko huo ulianza kwa bahati mbaya, kirusi-tafiti kilipovuja.

> Utafiti wa kipelelezi unapendelea zaidi maelezo kuwa mfumuko huo ulikuwa ni kuvuja kwa kirusi hicho sokoni, si nyama pori.



Kinachotofutisha utafiti huu na zilizotangulia au za kawaida, ni kuwa utafiti huu mpya, ni pamoja na kufuatilia taarifa za kidukuzi zilizochokuwa katika eneo la kuanza kwa maambukizi, yaani Jimbo la Hubei na hasa Jiji la Wuhan na viunga vyake, nchini China.

Ni soko lenye nyamapori za kila aina, ambako kimsingi ulianza mfumuko wa maambukizi, halitiliwi maanani tena kwani mfumo wa virusi vya Covid-19 umeonekana hauna tofauti na ule wa SARS ya mwaka 2012, iliyotokana na kula nyama ya popo.

Ila tofauti ni kuwa SARS-2 ina uwezo mkubwa zaidi wa kupenya kinga za mwili wa binadamu kuliko mwanzo na kwa maana hiyo, mfumuko wa maambukizi umekuwa tofauti kabisa na ilivyokuwa wakati wa SARS ya awali.

Kitaaluma, watafiti wanasema kuna maelezo ya kitafiti ya kutosha kuhusu mtiririko wa virusi vya popo kuchukua sura tofauti kwa hatua kadhaa na kujiambatanisha na mwili wa binadamu, katika tatizo (ugonjwa wa SARS) ya awali.

**KIULIZO KILIPO**

Suala ni mabadiliko gani na hatua gani za kubadili sura kimaumbile zilitokea kwa aina hiyo ya virusi, kuchukua sura ya ukali (uwezo wa kupitiliza) kushambulia mwili wa binadamu, hadi ukafikia uwezo huo wakati wa kuambukizwa mgonjwa wa kwanza wa Covid-19.

Ni hapo ambako watafiti, wanakosa mtiririko tofauti wa virusi vya popo kuanzia 2012 hadi 2019 ambao kwa njia hiyo ya mabadiliko au kubadili sura ya chembe zake hapa na pale inawezekana kuelezea nguvu hiyo mpya inatoka wapi.

Kutokana na mkwamo huo wa jinsi virusi vya 'kawaida' vya SARS vinageuka kuwa vya Covid-19 na kutokana na mazingira yenyewe ya wimbi la Covid-19 lilipoanzia, utafiti-jasusi ulianza.

Moja ya maeneo yaliyoanza kugunduliwa katika utafiti uliotangulia hasa baada ya taasisi za China, zikijitahidi kusaidia utafiti wa kupata chanjo ya Covid-19 kuchapisha mfumo mzima wa vinasaba vya Covid-19.

Ni hatua ambayo wataalamu Marekani, kwa mfano watoa hoja katika mtandao wa kibiashara na taaluma wa Bloomberg nchini humo wanakiri kuwa uchapishajii wa mfumo vinasaba wa Covid-19 uliotoka China ulikuwa ndiyo msingi wa kampuni kadhaa kuanza utafiti wa kina wa chanjo ya gonjwa hilo.

**MAJIBU YA UTAFITI**

Baadhi ya utafiti wa chanjo umeelekeza nguvu zake katika kukabiliana na chembe-pembe inayopenyeza chembehai za mwili au za mifumo ya kinga na nyingine zimeelekeza juhudi zake katika chembehai za ndani za mfumo mzima wa kirusi cha Covid-19, kuzuia mfumo wake kujinakili.

Ni mfumo wa maisha wa chochote chenye mwili ni uwezo wa chembehai zake kujinakili wakati wote, zidumu.

Sababu nyingine ya kulazimisha mwelekeo wa kufuatilia zaidi utafiti-jasusi ni mtiririko wa makosa ya kitaaluma au uratibishaji wa utafiti virusi vya SARS huko China na hasa katika kituo cha WVI (Wuhan Institute of Virology - Taasisi ya Utafiti Virusi ya Wuhan).

Watafiti wanaeleza mtiririko wa nyaraka na taarifa za kitafiti za eneo hilo katika taasisi tofauti za nchi hiyo na ndani ya WVI kwenyewe zinaonyesha mikingamo ya wazi kuhusu nini kinaendelea, nini kinafuatiliwa na nini kimeonekana, katika kipindi cha mwaka mmoja au zaidi hadi kufikia kufumuka kwa Covid-19 sokoni Wuhan.

Utafiti wa kipelelezi unapendelea zaidi maelezo kuwa mfumuko huo ulikuwa ni kuvuja kwa kirusi hicho sokoni, si nyama pori.

Jibu halisi halijawekwa sawa, mgonjwa wa kwanza alitokea ndani ya taasisi hiyo ya kitafiti, hivyo akaambukiza wengine alipofika sokoni, au kuna kifaa alichokuwa nacho chenye mguso wa virusi vyenye nguvu katika maambukizi dhidi ya binadamu, kutokana na kukarabatiwa kwa malengo mahsusi.

Eneo hilo pia limeleta utata, kwani serikali ya China inadaiwa haina dhamira ya kufungua milango kwa watafiti kufanyia kazi maambukizi ya kwanza kabisa kutoka maabara au sokoni tu. Pia, kuna maswali hapo, kama ni sokoni, aliyetokea maabara alipona (kama wanavyopona wengine) au la?

Wasiwasi mwingine miongoni mwa wachambuzi, ni kuwa China inataka mjadala mpana wa ushirikiano wa kimataifa kuhusu kupambana na Covid-19, ili kupata chanjo ya pamoja, sio utafiti wenye malengo ya 'ilikuwaje.'



# RC apiga 'stop' mkandarasi kulipwa

**Na Augusta Njoji,**
MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amekagua ujenzi wa barabara ya Pandambili hadi Mpwapwa iliyoathiriwa na mvua huku akiagiza Wakala wa Barabara nchini (TANROAD) kutomlipa mkandarasi hadi arekebishe ukuta wa daraja la Chinyasungwi alioupindisha.

Barabara hiyo iliyoathiriwa ni kutoka eneo Pandambili-Mlali-Mpwapwa hadi Nghambi, daraja la Chinyasungwi na eneo la Iyoma. Zaidi ya Sh. bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Akizungumza jana baada ya kukamilisha ukaguzi huo, Dk. Mahenge alimwagiza Kaimu Meneja wa TANROAD Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salome Kabunda, kutomlipa mkandarasi, Musons Engineering, hadi arekebishe ukuta huo.

"Mkandarasi huyu anatakiwa alipwe Sh. bilioni 1.109, lakini nikiangalia hapa naona kabisa ukuta mmoja wa ukingo wa daraja umepinda, lakini upana wa ukuta huo naona ni mwembamba ilhali eneo hili linapita maji mengi, nikuelekeze meneja usimlipe mkandarasi fedha hadi arekebishe," aliagiza.

Hata hivyo, aliagiza kuwapo na usimamizi katika maeneo yote ambayo ujenzi unaendelea ili makosa kama hayo na mengine yasijitokeze.

"Kama ukuta unatakiwa kujengwa kwa sentimita 30 ukipunguza hata sentimita mbili unaongelea kupunguza saruji, mchanga na ukipiga hesabu unaona kabisa fedha nyingi zinakuwa zimepotea, hivyo ni muhimu kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa karibu wakati wote," alisisitiza Dk. Mahenge.

Kadhalika, alimwagiza Mkurugenzi wa Bahati Investment anayejenga barabara kipande cha Iyoma kuongeza vitendea kazi na kufanya kazi usiku na mchana ili mvua isiathiri kazi inayoendelea.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alishukuru serikali kwa kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi katika maeneo hayo. Eneo hili la daraja la Chinyasungwi yanapita maji mengi, yakiwamo mengine kutoka mkoani Manyara. Katika mvua iliyonyesha mwaka jana, kuna kitongoji kilikuwa kisiwa, familia 22 zilikwama huko ikabidi tutafute boti kwa ajili ya kuwatoa. Uwapo wa daraja hili utasaidia sana kupunguza adha hii," alisema Shekimweri.

Alisisitiza suala la kuimarishwa kwa usimamizi katika maeneo yote yanayoendelea na ujenzi ili kazi inayofanyika iendane na thamani ya fedha iliyotolewa na serikali.



Mbeba mizigo wa Soko la Sabasaba jijini Dodoma akipita kwa shida kwenye njia iliyojaa tope iliyopo katikati ya soko hilo, kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ufumbuzi kero ya maji ndani ya siku 100

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mjini Dodoma (DUWASA) imejipanga kutatua kero ya maji kwa wananchi ndani ya siku 100 kwa kuchimba visima 10 vitakavyoongeza upatikanaji wa maji.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Aron Joseph, aliyasema hayo jana katika ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, kukagua maendeleo ya ujenzi wa miradi ya maji jijini hapa. Alisema kwa sasa uhaba wa maji uliopo ni lita za ujazo milioni 37 kwa siku.

"Katika kuhakikisha tunapunguza upungufu huo tayari tunachimba visima 10 katika maeneo mbalimbali ikiwamo Ihumwa na Zuzu, lengo letu katika siku hizi 100 tulizojipa tufanye kazi na wananchi wa Dodoma waone matokeo," alisisitiza.

Joseph alisema katika visima hivyo 10 wanavyochimba pembezoni mwa mji lengo likiwa kuhakikisha ndani ya mwezi huu viwe vimekamilika ili kazi ibaki kwenye kuviendeleza.

"Shughuli tunayoifanya ina lenga kupunguza tatizo la maji lililopo la lita za ujazo milioni 37 kwa siku. Kupitia visima hivi, tutapata maji lita za ujazo milioni 21 hadi 28 kwa siku, hivyo tutasaidia kupunguza uhaba wa maji Dodoma," aliongeza. Aidha, alisema kupitia chanzo kikuu cha maji cha Mzakwe, wanachimba visima vya maji vitatu ambavyo kila kimoja kitatoa maji si chini ya lita za ujazo 400,000 kwa saa kwa hiyo kwa vyote watapata maji sio chini ya lita za ujazo milioni 1.2 kwa saa.

Mhandisi Joseph alitaja mikakati mingine wanayoifanya ni kufufua visima vya maji vilivyotelekezwa ili kuongeza huduma ya maji kwa wananchi.

"Mpaka sasa tumeshavitambua visima 11 katikati ya mji, na dhamira yetu ni kuvifufua visima hivyo vya zamani ili visaidie kutoa huduma ya maji kwa wananchi na hivyo kupunguza upungufu wa maji uliopo," alisema.

# Vijana wapewa elimu kujiletea maendeleo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MABADILIKO ya fikra na ubunifu wa miradi yenye tija itawakomboa vijana kutoka katika umaskini badala ya kukaa vijiweni na kulalamika uchumi mgumu.

Mwinjilisti Festo Machela wa Kanisa Kuu la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika Dodoma, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na vijana wa kata ya Nzuguni jijini hapa.

Kutokana na ukweli huo, aliwataka kubadilisha mwelekeo wa maisha yao badala ya kuinyoshea serikali vidole kwa kutowapatia ajira.

Alisema vijana ni nguvu kazi kubwa katika taifa na hakuna ambaye atapata fedha za bure huku akiwa wamekaa vijiweni, na majumbani.

"Mnatakiwa kutambua wajibu wao wa kubadilisha mwelekeo huo na kubuni miradi ambayo itakayowaingizia kipato," alisisitiza.

Pia aliwataka vijana hao mwaka huu uwe wa mafanikio kwao kwa kufanya kazi kwa bidii huku wakiibua miradi mbalimbali hata kama mwaka jana hawakufanikiwa.

"Pamoja na mambo mengine, ni wajibu wa kila kijana wa Kitanzania kuhakikisha anajipanga kufanya kazi kwa bidii kubwa kwa ubunifu badala ya kukaa vijiweni na kubishania juu ya vitu ambavyo havina tija juu ya maisha," alisema.

"Ni wakati wa kufanya kazi kweli na kwa bidii kubwa na isiwepo sababu ya kufanya kazi kwa ulegevu maana hata maandiko ya Mungu yanasema apandaye haba atavuna haba, apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu," aliongeza.

Aidha, alisema Tanzania haiwezi kufikia uchumi wa kati wa juu kama vijana wake watakuwa wavivu, ombaomba na wasiojitambua na wanaotegemea misaada.

Mwinjilisti huyo aliwataka wahitimu wa elimu ya juu kuwa chachu ya maendeleo kwa kubuni miradi yenye tija ya kujiajiri badala ya kusubiri ajira serikalini, huku akiwaomba Watanzania kuendelea kuliombea taifa pamoja na kufanya kazi kwa bidii na uadilifu zaidi.

Alisema ili kuwa na taifa lenye viongozi waadilifu ni muhimu pia watu wake wawe waombaji kwa ajili ya nchi yao.

"Huwezi kuwa na taifa bora kama si wacha Mungu na kama viongozi watakuwa wacha Mungu na kujawa na hofu ya Kimungu, ni wazi kuwa vitendo vya uonevu, ulaji rushwa, ufisadi na unyanyasaji havitakuwapo," alisema.





# Mbunge atamba kutatua kero maji

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MBUNGE wa Kyela, Ally Kinanasi, amewahakikishia wananchi wa wilaya hiyo kuwa kipindi cha uongozi wake atahakikisha wanapata maji ya uhakika ya bomba.

Kinanasi aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye ziara ya kukagua vyanzo mbalimbali vya maji yanayotumika wilayani humo ambavyo vingi vinapatikana katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

Alisema serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Kyela pesa nyingi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi mingi na kwamba baadhi ya miradi hiyo imekamilika na mingine ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mbunge huyo alisema ili miradi inayotekelezwa na serikali iwe na faida kwa wananchi na idumu kwa muda mrefu, ni lazima kila mwananchi ashiriki kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji ikiwamo kutokata miti kwenye vyanzo hivyo.

"Tuna miradi mingi ambayo asilimia kubwa ya vyanzo vyake vipo Busokelo. Sasa ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunavitunza vyanzo hivi kwa kuvitembelea mara kwa mara ili tuwe na uhakika wa kupata maji muda wote," alisema Kinanasi.

Alizitaka jumuiya za watumia maji wilayani humo kuhakikisha zinakusanya mapato ya kutosha matengenezo ya baadhi ya vifaa kwenye miradi hiyo yawe yanafanyika mara kwa mara.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, waliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maji ambayo waliahidiwa na madai kuwa kwa sasa huduma hiyo ipo kwa kiwango kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa hawana uhakika wa huduma hiyo.

Joseph Mwakifuna, mkazi wa mji wa Ipinda, alisema awali walikuwa wanategemea sana maji ya kwenye visima ambayo usalama wake ni mdogo kwa afya zao lakini sasa hivi wanatumia majisafi ya bomba.

Alisema kabla ya maji ya bomba kuanza kutumika, mara nyingi wananchi walikuwa wanaumwa matumbo na mlipuko wa kipindupindu ulikuwa unawasumbua hasa kipindi cha mvua ambapo maji machafu yalikuwa yanaingia kwenye visima.

"Sasa hivi maji ya visima tunayatumia kwa ajili ya kufulia nguo na kuoga, hakuna tena kunywa kwa sababu tuna maji safi ya mabomba na tunahamasishwa kila mwenye uwezo avute bomba nyumbani kwake," alisema Mwakifuna.

Alisema hata katika Kituo cha Afya cha Ipinda ambacho ni miongoni mwa vituo bora vya afya katika Mkoa wa Mbeya, maji yalikuwa ni tatizo kubwa awali lakini kwa sasa yapo ya kutosha.




Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Jerome Ngowi, akiwaonyesha waandishi wa habari baadhi ya silaha ambazo jambazi aliyeuawa kwenye majibizano ya risasi na polisi kwenye kituo kikuu cha mabasi cha jijini Mbeya usiku wa kuamkia juzi, aliyokuwa anaitumia. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mtuhumiwa ujambazi auawa kwa risasi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MTU mmoja asiyefahamika jina wala anakotokea, anayedhaniwa kuwa ni jambazi, ameuawa kwa kupigwa risasi katika majibizano ya risasi na polisi mkoani hapa akiwa na wenzake watano katika kituo kikuu cha mabasi cha Mbeya.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Jerome Ngowi, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi saa 6:10 usiku baada ya wananchi kutoa taarifa za siri kuhusu watu hao.

Alisema baada ya jeshi hilo kupata taarifa hizo, lilituma kikosi maalumu cha kupambana na uhalifu ambacho baada ya kufika katika eneo hilo, wahalifu hao walishtuka kuwa wanafuatiliwa ndipo wakaanza kutimua mbio.

Ngowi alisema wakati wanatimua mbio, mmoja wao ambaye alikuwa na silaha, alianza kurusha risasi ndipo askari wakajibu mapigo kwa kumrushia risasi ambazo zilimjeruhi vibaya na wakati anapelekwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya alifariki dunia. Kamanda Ngowi alisema baada ya kumpekua, walikuta bunduki moja aina ya shotgun iliyotengenezwa kienyeji, risasi 12 za shotgun na maganda mawili ya risasi.

"Wenzake walikimbia na kutokomea kusikojulikana, lakini tunaendelea na msako. Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na marehemu anakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 30 na 35," alisema. Katika tukio lingine, Kamanda Ngowi alisema jeshi hilo linawasaka watu wawili, wakazi wa Matundasi wilayani Chunya kwa tuhuma za kufanya mauaji. Aliwataja watu hao kuwa ni Juma Sunzima na Marry Daimon, ambao wanadaiwa kumuua Juma Kitemango (48) ambaye alikuwa mume wa Marry.

Alisema Kitemango aliuawa na watu hao kwenye ugomvi wa kimapenzi baada ya kumfumania Sunzima na mkewe wakifanya mapenzi nyumbani kwake na wakati wa mapambano watuhumiwa walimuua kwa kumkata na kitu chenye ncha kali na kumchoma jicho la kushoto na utosini.

"Katemango alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu kwenye zahanati ya Matundasi, lakini inasemekana kuwa yeye na mkewe walikuwa na ugomvi wa muda mrefu," alisema Kamanda Ngowi.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika zahanati hiyo na kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu huku wahusika wakiendelea kusakwa ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Wakati huo huo, alisema mtoto mmoja aliyefahamika kwa jina la Bradon Wiseman (4) mkazi wa Kijiji cha Mpandapanda wilayani Rungwe, alifariki dunia, huku mwenzake Alen Kaduma (6) akijeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili wake baada ya nyumba walimokuwa wamelala kuwaka moto. Alisema chazo cha moto huo ni kibatali ambacho walikiacha kikiwaka kuunguza nguo zilizokuwa zimening'inizwa na kisha kusababisha madhara hayo.

# Watembea kilomita saba kusaga nafaka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa vijiji vya Shongo na Igale vilivyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatembea umbali wa zaidi ya kilomita saba kwenda kusaga nafaka katika Mji wa Mbalizi kutokana na vijiji hivyo kukosa huduma ya umeme.

Vijiji hivyo vinadaiwa kutofikiwa na huduma hiyo liche ya serikali kuendelea kusambaza nishati hiyo kwenye vijiji mbalimbali nchini kupitia Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA).

Wakizungumza wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, katika vijiji hivyo, wananchi hao waliiomba serikali kuwasaidia kupata huduma hiyo haraka ili kuwapunguzia adha ya kuzifuata huduma zinazotumia nishati hiyo Mbalizi.

Diwani wa Kata hiyo, Michael Mwanibhungu, alisema wananchi wa vijiji hivyo wanahitaji sana huduma hiyo kutokana na matatizo ambayo wanakabiliana nayo.

Alisema wana shughuli nyingi ambazo zinahitaji uwepo wa nishati hiyo ikiwamo kuchaji simu, kuchomelea pamoja na matumizi mengine ya nyumbani.

"Kuna watu wamenunua mashine wanazo ndani, lakini hawawezi kuzisimika kwa sababu umeme haupo, sasa tunaiomba serikali iharakishe mchakato wa kuleta umeme kwenye vijiji hivi ili tuondokane na adha hii," alisema Mwanibhungu.

Alisema umeme ni kichocheo kikubwa cha maendeleo vijijini kutokana na kuwa moja ya njia za kuwazuia vijana kukimbia maeneo hayo na kukimbilia maeneo ya mjini hali ambayo huwa inazorotesha nguvu kazi kwenye maeneo hayo.

Naye Vumilia Mwajanga alisema mbali na huduma ya mashine za kusaga pia wanawake huwa wanatamani kuanzisha viwanda vidogo, lakini wanashindwa kutokana na kukosa nishati.

Alisema wamekuwa wakipata mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali lakini wanashindwa kuyatumia hasa kutengeneza sabuni, kuanzisha saloon na vwanda vingine. Akizungumzia tatizo hilo, Njeza alisema jimbo hilo mpaka sasa lina jumla ya vijiji 40 ambavyo bado havijafikiwa na huduma ya umeme vikiwemo vya Shongo na Igale vilivyoko katika Kata ya Igale.

Njeza alisema serikali imeshaviingiza vijiji hivyo kwenye bajeti ya mwaka huu ili na vyenyewe vipatiwe umeme na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu jimbo zima litakuwa na umeme.

Vijiji hivyo, alisema viko jirani na mjini, hivyo vinaona faida ambazo wenzao wanazipata hali ambayo inawafanya wawe na shauku kubwa ya kuunganishiwa huku akidai kuwa huduma hiyo inahitajika kwenye shule na zahanati.

"Nimeongea na Waziri wa Nishati na akanihakikishia kuwa vijiji vyote vitapata umeme ndani ya muda mfupi ujao na sasa hivi wanaendelea na mchakato wa makandarasi, kwa hiyo nawaomba wananchi wawe na subira," alisema Njeza.



## HABARI ZANZIBAR

# Mwinyi aahidi kulinda amana ZSSF

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kufanya kazi kwa karibu na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuhakikisha amana zote za wanachama zinasimamiwa ipasavyo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika hotuba yake ya ufunguzi wa jengo jipya la Hifadhi Building lililoko Tibirinzi, Wilaya ya Chakechake, Mkoa wa Kusini Pemba, ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Katika hotuba hiyo, Rais Mwinyi alisema ni jukumu la serikali kuhakikisha inachukua hatua zinazofaa na kwa wakati katika kuhakikisha mfuko huo unaendelea kuimarika, unaongozwa na kusimamiwa na viongozi walio makini na wanaojiepusha na vitendo vya ubadhirifu, rushwa na wizi.

Alisisitiza kwamba serikali itahakikisha wanachama wa mfuko huo wanaishi bila kuwa na wasiwasi wa hatima ya amana wanayowekeza ambayo mara nyingi huwa ni tegemeo kubwa katika maisha ya wafanyakazi baada ya kustaafu.

Dk. Mwinyi aliwataka viongozi kuhakikisha fedha inayowekezwa, inazalisha na shughuli zote za uendeshaji wa taasisi hiyo zinafanywa kwa weledi, umahiri na umakini mkubwa.

Alisema kuwapo kwa majengo ya ofisi za kisasa ni hatua muhimu katika juhudi hizo za kuvutia wawekezaji kisiwani Pemba.

Alisema kazi kubwa imefanywa na Serikali ya Awamu ya Saba kuimarisha mazingira ya kufanya kazi kisiwani Pemba, ambapo majengo mengi ya serikali yamejengwa na mengine yamefanyiwa matengenezo makubwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Katika hotuba yake hiyo, Rais Mwinyi pia aliwahimiza viongozi wa (ZSSF) kuhakikisha taratibu za ukodishaji wa maduka yaliyomo katika maduka mapya ya Michenzani Mall na jengo la Thabit Kombo kwa kuwa ni kipindi kirefu tangu majengo hayo yalipozinduliwa rasmi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango), Jamal Kassim Ali, alisema kukamilika kwa ujenzi huo ni mafanikio makubwa kwa kuwa kutaongeza ufanisi na mapato.

Alisema kukamilika kwa jengo hilo kunatokana na ushirikiano wa Mfuko wa ZSSF, Wizara na Bodi ya Mfuko huo sambamba na ushauri mkubwa uliokuwa ukitolewa na Rais juu ya mfuko huo, huku akieleza taasisi za serikali kuwa makini katika kutekeleza miradi kama hiyo.

Alisema kwamba fedha zilizotumika ni michago ya wanachama wa ZSSF, hivyo ni vyema zikarudi na kupata tija kwa wanachama wa mfuko huo huku akiwataka wale wote watakaokodi jengo hilo, kulipa fedha zinazotakiwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango), Khamis Mussa Omar, alisema ZSSF iliamua kujenga jengo hilo jipya la kisasa linaloendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye, akibainisha kuwa mkataba wa ujenzi ulitiwa saini Julai 4, 2019 baina ya ZSSF na Kampuni ya Kizalendo ya Quality Building Contractors baada ya kampuni hiyo kuwa mshindi wa zabuni.

Ujenzi ulianza rasmi Agosti Mosi 2019 na utalikiwa kukamilika Julai 31, 2020, lakini kutokana na vikwazo vilivyobainika wakati wa ujenzi na athari ya maradhi ya corona, ulikamilika rasmi Oktoba mwaka jana.

Jengo hilo la ghorofa tatu, limegharimu jumla ya Sh. bilioni 7.9 zimetarajiwa kutumika katika ujenzi wa jengo hilo ambalo hadi sasa, jumla ya Sh. bilioni 5.3 zimeshalipwa kwa mkandarasi.



Prof. Razack Lukina Mtaalamu wa Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) akiwasilisha mada kuhusiana na uchumi wa buluu wakati wa kongamano la Jumuiya za Chama Cha Mapinduzi za UWT, UVCCM na Wazazi, lililofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Daktari: Jamii iendelee kujilinda corona

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

DAKTARI Sanaa Said wa Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, ameitaka jamii kuendelea kuchukua tahadhari na kufuata miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Afya, ili kujikinga na maradhi ya mlipuko ikiwamo corona.

Alitoa hadhari hiyo jana wakati wa mafunzo ya siku moja ya kutengeneza ujumbe kuhusu kujikinga na virusi vya corona kwenye ukumbi wa Mtakwimu wa Serikali uliopo Mazizini visiwani hapa.

Alisema hatua ya wananchi kujikinga na kuendelea kuchukua tahadhari juu ya magonjwa ya mlipuko, itasaidia jamii kubaki salama na kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Dk. Sanaa alisema licha ya kuwa sasa Zanzibar hakuna maradhi hayo ya corona, jamii inasisitizwa kuendelea kuchukua tahadhari pamoja na kujikinga kwa kuwa baadhi ya nchi maradhi hayo yapo na wageni kutoka sehemu tofauti wanaingia ndani ya visiwa hivyo.

Alitumia fursa hiyo kuisisitiza Taasisi ya Panje Project kuendelea kuiunga mkono serikali katika kutoa elimu hiyo kwa kuwa itachochea jamii kujikinga na kufika haraka vituo vya afya pale wanapoona wana dalili ya maradhi hayo.

"Afya ni kitu muhimu kwa binadamu kwani ndiyo chachu ya kuwawezesha kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo na kuchochea ukuaji wa uchumi," alisema. Meneja wa Taasisi hiyo Muhammad Suleiman Said, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo ili kuiunga mkono serikali juu ya kupambana na ugonjwa huo.

Akizungumzia mkutano huo, alisema wameamua kufanya mkutano huo ili kupata ujumbe ambao watapeleka kwa jamii kwa lengo la kuchukua tahadhari juu ya kujikinga na virusi vya corona.

Alifahamisha kwamba elimu hiyo itatolewa kwa njia ya vitendo ambayo watapita katika vyuo vya madrasa, skuli na kuweka mikutano kwa wanajamii ili kuwakumbusha kuendelea kuwa na tahadhari.

Meneja huyo alisema katika kufanikisha suala hilo, watahakikisha wanashirikiana na wadau mbalimbali wa serikali na binafsi ili kuona lengo linafanikiwa kwa asilimia kubwa.

"Asilimia kubwa ya wananchi hivi sasa wamejisahau kwa kuona kwamba maradhi hayo hamna, lakini mipaka iko wazi na wageni wanaingia, hivyo ni jamii ikumbushwe ili kuchukua tahadhari," alisema.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliandaliwa na taasisi ya Panje kupitia mradi wa ushiriki wa afya ya jamii juu ya kupunguza athari za maradhi ya mlipuko ikiwamo maradhi ya corona katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.

# Mbunge abaini shida malezi ya watoto

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Unguja, amewataka wazazi na walezi kushirikiana na walimu wa madrasa ili kuwalea watoto katika misingi ya dini ya Kiislam na kupata vijana wenye malezi bora, upendo, uzalendo na kujenga taifa bora lisilo na vitendo vya udhalilishaji.

Mwatumu Dau Haji alitoa rai hiyo wakati wa hafla ya kukabidhi vitendea kazi kwa Madrasatul Sanaa Muntahal-kalam huko Ukongoroni, akisema dini ina mchango mkubwa katika kuwajenga watoto kiimani na hatimaye kupata kizazi chenye nidhamu nchini.

Alisema elimu ya dini hasa Qur-an, ina maelekezo mazuri na haikuacha kitu katika suala la malezi na namna jamii inavyotakiwa kuishi, hivyo amewataka wanajamii kuifuata ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji hasa kwa watoto ambao wamekuwa waathirika wakubwa wa kadhia hiyo.

"Ikiwa tunataka vitendo vya udhalilishaji viondoke, basi tufuate misingi na miongozo iliyomo katika kitabu cha Qur-an na mafundisho ya Mtume Muhammad (S.A.W). Ni vyema wazazi, walimu na walezi kuzitumia madrasa katika kutoa malezi bora," alishauri.

Katika hafla hiyo, mbunge huyo alikabidhi mabusati na kompyuta kwa madrasa hiyo ili kuiendeleza.

Mbunge huyo pia alipata fursa ya kukutana na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kusini Unguja na alichangia Sh. milioni mbili kwa ajili ya shughuli za kichama.

Aliwataka viongozi wa chama hicho Mkoa wa Kusini Unguja kutumia fedha zinazotolewa na viongozi wa chama hicho kwa maslahi ya chama na jumuiya zake.

Mbunge huyo pia alizindua kikundi cha Vikoba Wilaya ya Kusini Unguja na kuchangia Sh. milioni mbili kwa ajili ya kukiendesha kikundi hicho ili kujikwamua kiuchumi.

Wawakilishi wa Viti Maalum Wanawake Mkoa wa Kusini Unguja walichangia Sh. milioni mbili na nusu katika Kikundi cha Vikoba Wilaya ya Kusini Unguja.

Akizungumza kwa niaba ya wanakikundi hicho, Salama Ali Hamadi, amesema lengo kuu la kikundi hicho ni kuweka na kukopa pesa ili kupunguza umaskini kwa kufanya biashara na kusomesha watoto.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,

Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.

E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 989 CMC AINA YA PIAGGIO APE. KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.TAARIFA YA POLISI: KAH/TR/RB/05/2021.

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### KUITWA SHAURINI MDAIWA
### (MCA/63)

Mahakama ya Mwanzo…Ya..MBALIZI……Wilaya…ya …………MBEYA……………….

NAMBARI ……143……YA…….2020………………………………………………

MDAI…FADISHENI… KAMWELA……………………………………………………

DHIDI ….YA…

MDAIWA……REBEKA MWAKLA……………………………………………………

KWA:… …REBEKA MWAKWILA………………………………………

K.K…KIONGOZI WA …SERIKALI… MTIMBILA …MALINYI… MOROGORO……………………………………….

Kwakua Mdai/Wadai Ameleta /Wameleta Madai Yake/Yao………………………

JUU…YA…MADAI…YA…KUACHANA…(TALAKA)…………………………

KwahiyoUnahitajiwa/Anahitajiwa Kuhudhuria Binafsi katika Mahakama hii siku ya Tarehe 14/01/2021 Saa 2:30 Asubuhi,kwa kujibu Madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa Shauri hilo,nilazima kuleta Shahidi Wako/Wenu na Hati zote zinazohusu Shauri hilo kwa ajili ya Kujitetea katika Shauri hilo.

Angalia kama Hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa Hukumu kuwa Umeshindwa/Ameshindwa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama leo hii Tarehe 30/12/2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MBALIZI-MBEYA

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
### (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2
### Katika mahakama ya mwanzo

MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;06/2021

Ombi la **MARY SILVERIUS HAULE**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **THEODOSY JOSEPH MSOGOYA**.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **12/02/2021** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/01/2021.

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
### (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2
### Katika mahakama ya mwanzo

MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;07/2021

Ombi la **SAUDA JUMA KAPELA**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MWADAWA OMARY MAPANGA.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/02/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/01/2021.

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### KUITWA SHAURINI MDAIWA
### Mahakama ya wilaya ya DODOMA MJINI
### Wilaya ya DODOMA

MADAI NAMBARI 274/2020

MDAI **ZABRON MROBEZI**

MDAIWA **ANNA JOHN RUSAKU**

Kwa **ANNA JOHN RUSAKU**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba

MADAI YA TSH **2,018,000/=**

Hivyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 21/01/2021 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 30/12/2020.

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO

### UPOTEVU WA KADI YA PIKIPIKI

**EDWARD JOSEPH NGOGO** MTAJWA HAPO JUU ANATANGAZA KUPOTELEWA KADI YA PIKIPIKI AINA YA BOXER USAJILI NAMBA **MC.113.BYY** TAARIFA YA POLISI NI KUMB **No.MBE/TUK/RB/232268/2019 CONTOROL No.991088985750** KWA YEYOTE MWENYE TAARIFA APELEKE KITUO CHOCHOTE CHA KARIBU NAYE.

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GABRIELA FIRMIN SUKUMS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T410CXQ Toyota IST** colour SLIVER Chasis namba **NCP650033637** Engine namba **1NZ9215876** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. TAARIFA YA Polisi: **MWA/NYA/RB/2547/2021**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LEONARDD MAGUTA KUNZA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 805 DCR** AINA YA TOYOTA KLUGER STATION WAGON YENYE ENGINE **NO 2AZ1744403** NA CHASSIS NO ACU 250036720 KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI **TAARIFA YA POLISI KAH/TR/RB/03/2021**

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
### (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2
### Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;03/2021**

**Ombi la LINDA C NGIDO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu KIHARA NGIDO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/01/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/01/2021.

Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini

MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES
P.O.BOX 429 DODOMA – TANZANIA
OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9
0715170553 / 0756011439

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Ninautangazia umma kuwa, kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo Chamwino mjini wilaya ya Dodoma nitauza kwa mnada wa hadhara nyumba moja iliyopo kwenye kiwanja nambari **15 kitalu K Kisasa North** ndani ya Jiji la Dodoma mali ya **FABIANI WENGA** ili kufidia deni analodaiwa na **IMARIKA FINANCIAL SERVICES.** Mnada utafanyika mahali nyumba ilipo na nyumba itauzwa kama ilivyo, siku ya tarehe **24/01/2021 saa nne 4:00 asubuhi.** karibuni nyote, usisite kuwasiliana nasi kwa maelekezo zaidi kupitia **simu namba 0735 170 553 (DALALI WA MAHAKAMA)**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

ROCK TAKERS LTD

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**SHAURI LA MADAI NA. 296/2020**

**AMOS STANSLAUS MASUNGA ……………………. MDAI**
**DHIDI YA**
**THOMAS MASHIMBA………………………….MDAIWA**
**EXCUTION NO. 11/2010**
**JACKSON ELIAS MASHAMBO……………… PETITIONER**
**VERSUS**
**JOSEPH JUMA BUJIMILE ……..JUDGEMENT DEBTOR**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA NYAMAGANA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MFAWIDHI TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA AMBAZO NI NYUMBA NA MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ZILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA PLOT 725 | NYAKATO | 20/01/2021 SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA |
| 2 | KIWANJA | BUSWELU-ILALA CENTER | 20/01/2021 SAA 8 MCHANA NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA | KISESA-KANYAMA CENTER | 21/01/2021 SAA 4 ASUBUHI NA KENDELEA |
| 4 | KIWANJA | NYAMHONGOLO | 21/01/2021 SAA 6 MCHANA |
| 5 | NYUMBA | ISAMILO-KASKAZINI 'A' | 19/01/2021 SAA 8 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOAFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE, KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGINA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0713 342969/ 0766 342969**

ROCK TAKERS LTD

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**CIVIL CASE NO. 71/2019**

**ADMIRE OIL LIMITED ………………………..PLAINTIFF**
**VERSUS**
**PETROLUX SERVICE STATION……………….DEFENDANT**
**DC MATRIMONIAL CASE NO. 04/2019**
**GABRIEL MASUMBUKO JOSEPH……………PLAINTIFF**
**VERSUS**
**PERPETUA CHAUSIKU GEORGE ……..DEFENDANT(S)**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA NYAMAGANA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MFAWIDHI TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA AMBAZO NI NYUMBA, KIWANJA NA GARI, NA MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ZILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | VIWANJA | BUZURUGA Kiwanja Na. 449 and 450 Kitalu G Nyakato Area. | 30/01/2021 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | GARI – ISUZU lenye namba T 278 ALN | Mwanza Pasiansi | 30/01/2021 SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA |
| 4 | NYUMBA | NYAKATO- MAHINA | 22/01/2021 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOAFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE, KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGINA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0713 342969/ 0766 342969**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# 21 wafa wakishambuliwa na waasi ADF Mashariki

**Beni,** DRC

WATU 21 wameuawa Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), baada ya kushambuliwa na waasi wa kundi la ADF, ambalo limelaumiwa kusababisha vifo vya mamia ya watu, mwaka jana.

Ripoti kutoka Jeshi la Umoja wa Mataifa (MONUSCO), limesema kuwa, watu hao wameuawa katika Kijiji cha Mwenda, eneo la Rwenzori.

**Watu 10 wamejeruhiwa na wengine hawajulikani waliko.**

Hata hivyo, kiongozi wa eneo hilo, Donat Kibwana, alisema ni watu 22 waliopoteza maisha, 10 kati yao ni wanawake.

Kibwana alisema kuwa watu 10 walijeruhiwa katika shambulizi hilo dhidi ya raia katika Wilaya ya Beni.

"Watu 10 wamejeruhiwa na wengine hawajulikani waliko," alisema Kibwana.

Mauaji hayo yanatajwa ya pili ndani ya wiki moja, tangu mwaka mpya wa 2021 ulipoanza, baada ya mengine kutokea katika kijiji cha Tingwe.

Kundi la waasi wa ADF, limelaumiwa kusababisha vifo vya watu karibu 800 mwaka 2020, katika Jimbo la Kivu Kaskazini na Ituri, maeneo ambayo yanapakana na Uganda. **RFI**



Magari yakiwa yamejipanga ili kuwafanyiwa uchunguzi wa maambukizi ya virusi vya corona, watu waliomo kwenye magari Uwanja wa Dodger, Los Angeles, Marekani. Juzi nchi hiyo, ilirekodi vifo vya corona 4,000, kulingana na Chuo Kikuu cha Johns Hopkins. **PICHA: REUTERS**

## Upinzani CAR wataka matokeo ya uchaguzi urais yafutwe

**Bangui,** CAR

WAGOMBEA 10 wa upinzani katika uchaguzi wa rais uliofanyika katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), wametoa wito wa pamoja, kutaka matokeo ya uchaguzi huo yafutwe.

Wagombea hao, wanadai kulikumbwa na hitilafu nyingi.

Mwanzoni mwa wiki hii, Tume ya Uchaguzi ya nchi hiyo, ilimtangaza Rais Faustin Archange Touadera, kuwa mshindi wa uchaguzi huo wa Desemba 27, mwaka jana, kwa asilimia 53.92 ya kura zilizopigwa.

Ushindi huo ni iwapo, utathibitishwa na mahakama ya juu ya taifa hilo, ikimaanisha kuwa hakutakuwapo duru ya pili ya upigaji kura.

Juzi, mgombea wa nafasi ya pili aliyepata asilimia 21.01 Waziri Mkuu wa zamani, Anicet Georges Dologuele, alisema tume hiyo, imechukua hatua ya kuwapuuza wapigakura karibu 950,000 waliozuiwa kupiga kura kutokana na ghasia za makundi yenye silaha.

Mshindi wa nafasi ya tatu, Martin Ziguele, alisema hayapi umuhimu wowote, matokeo yaliyotangazwa na tume akiyataja kama matokeo ya aibu kwa nchi. **DW**

## UNHCR yapokea wakimbizi 800 kwa wiki moja kutoka Tigray

**Geneva,** USWISI

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), limeandikisha wakimbizi wapya katika mpaka wa Sudan na Ethiopia, takriban 800 waliovuka mpaka kutoka eneo la Tigray.

Wakimbizi hao walitokea nchini Ethiopia na kuingia Mashariki mwa Sudan, siku chache za mwaka huu wa 2021.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya simu, mjini Geneva Uswisi, Msemaji wa UNHCR, Andrej Mahecic, alisema tangu Novemba mwaka jana, zaidi ya wakimbizi 56,000 kutoka Ethiopia walifungasha virago kukimbia machafuko na kuingia nchi jirani Sudan.

UNHCR, limesema wakimbizi wanaowasili wanafika na nguo pekee walizovaa, wakiwa wamechoka na dhaifu baada ya safari ya siku kadhaa.

Linasema, asilimia 30 ya wakimbizi ni chini ya umri wa miaka 18 na asilimia tano wana umri wa zaidi ya miaka 60. **UN**

## Museveni amteua mwanajeshi kusimamia usalama Uganda

**Kampala,** UGANDA

RAIS Yoweri Museveni wa Uganda, amemteua Meja Jenerali Kayanja Muhanga, kuwa Mratibu wa masuala ya Usalama, nchini humo.

Naibu Msemaji wa Jeshi, Luteni Kanali Deo Akiiki, aliiambia BBC kwamba, Meja Jenerali Muhanga, atakuwa mratibu wa operesheni za vitengo vyote vya usalama.

"Ni kweli kwamba Brigedia Kayanja Muhanga, amepewa nafasi ya kuratibu vikundi vyote vya usalama kwa madhumuni ya kuunganisha shughuli ya usalama wa pamoja hususan katika mji wa Kampala na nchi yote," alisema Akiiki.

"Hiyo ina maana kwamba atakuwa kiunganishi kati ya kikosi cha polisi, jeshi na idara ya ujasusi."

Rais Museveni, aliweka shinikizo kwa polisi wa mji wa Kampala, ambao karibia watawaliwe na ghasia za wahalifu.

Tangu uzinduzi wa kamera za CCTV, kituo kinachohusika na jeshi pamoja na maofisa wa polisi, kilibuniwa katika kituo cha polisi cha Kampala.

Kulingana na gazeti la the Monitor, kunapotokea tishio lolote Meja Jenerali Samuel Kawagga, Kanali Keith Katungi, Kamanda wa Polisi mji wa Kampala, Moses Kafeero na kamanda wa polisi wanaosimamia wanajeshi hukutana katika kituo hicho cha kati ili kutafuta mbinu ya kuangazia tatizo lililopo. **BBC**

## Ujerumani yarefusha mapambano corona

**Berlin,** UJERUMANI

WANASIASA nchini Ujerumani wamekubaliana kurefusha hatua kali za kuzuia kasi ya maambukizi ya virusi vya corona, hadi Januari 31, mwaka huu.

Hatua hizo zilitangazwa na Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, jana usiku, baada ya mkutano na wakuu wa majimbo ya shirikisho la Ujerumani.

Kulingana na hatua hizo, shule zitaendelea kufungwa, na watu katika wilaya zenye viwango vikubwa vya maambukizi hawataruhusiwa kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 15 kutoka nyumbani kwao, bila sababu ya lazima.

Kansela Merkel, alimtetea Waziri wa Afya, Jens Spahn anayekabiliwa na ukosoaji kutokana na mapungufu katika usambazaji wa chanjo ya corona, akisema anafanya kazi nzuri. **DW**

# GIROUD AJIANDAA KUBAKI CHELSEA




**LONDON,** England

OLIVIER Giroud anatarajiwa kuendelea kukaa Chelsea katika dirisha hili dogo la Januari licha ya miamba ya Serie A, Juventus kuonyesha kumhitaji.

Mshambuliaji huyo wa Blues atakaa London kwa sasa, lakini alama za maswali zinabaki juu ya siku zijazo za baadaye pale Stamford Bridge.

Frank Lampard ameonyesha nia yake ya kutaka kuendelea kuwa na raia huyo wa Ufaransa pale Stamford Bridge kwa miezi mingine sita wakati presha inakuwa juu ya nafasi yake ya kuongoza klabu hiyo.

Mkataba wa Giroud unamalizika Juni 2021 na hakuna kifungu maalum ambacho Chelsea inaweza kuomba kumwongezea, baada ya mwaka jana kutumia kipengele cha kumbakiza kwa mwaka mwingine.

Kwa hiyo 'The Blues' itahitaji kukubali makubaliano mapya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 ili aendelee kusalia katika klabu hiyo, na Giroud amezungumza na Le Dauphine Libere juu ya hali yake.

Alisema: "Tamaa ni kushinda kitu na Chelsea msimu huu. Kazi yangu yote, kwa muda mfupi, naiona Chelsea. Sasa tunajua kuwa mambo yanaenda haraka sana katika mpira wa miguu, kwa uzuri na ubaya. Nataka kuweka kichwa vizuri na nizingatie zaidi kwenye uwanja.

# EPL kutosimama kwa corona

**LONDON,** England

LIGI Kuu England imebainisha kwamba, michezo yake itaendelea kama kawaida licha ya kurekodi visa vingi zaidi vya maambuzi ya virusi vya corona.

Kwenye Ligi Kuu England kumerekodiwa visa vipya 40 vya virusi vya corona katika raundi nyingine ya hivi karibuni wakati wa upimaji, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya wiki iliyopita.

Matokeo ya kutia wasiwasi yanakuja siku moja baada ya serikali ya Uingereza kutangaza kuzuiliwa kwa kitaifa (Lockdown) kwa nia ya kudhibiti kuenea kwa virusi, baada ya kuongezeka zaidi.

Ligi Kuu ilipanua upimaji wake wa kujaribu mara mbili kwa wiki na majaribio yaliyofanywa kwa wachezaji na wafanyakazi kati ya Desemba 28 hadi 31, mwaka jana yalirudisha visa vipya 28, na 12 zaidi wakati wa zoezi la pili la upimaji, kati ya Januari Mosi hadi 3, mwaka huu.

Kiwango cha juu cha wiki kilichopita kilikuwa na matokeo 18 mazuri wakati wa wiki iliyotangulia, kutoka Desemba 21 hadi 27.

Katika taarifa yake ya jana, Ligi Kuu ya England imesema: "Pamoja na idadi ndogo ya vipimo katika idadi kubwa za klabu, ligi inaendelea na michezo yake ichezwe kama ilivyopangwa."

Ratiba tatu za timu za juu – mechi ya Manchester City na mechi za Everton na Fulham dhidi ya Tottenham na Burnley ziliahirishwa wiki iliyopita.

# Ferdinand hajali Pogba akiondoka



**MANCHESTER,** England

RIO Ferdinand amesema hajali ikiwa Paul Pogba ataondoka Manchester United wakati wa majira ya joto, kwani anaamini klabu inapaswa kumtolea macho nyota wa Aston Villa, Jack Grealish.

Beki huyo wa zamani wa England amelinganisha uwezo wa Grealish na ule wa Lionel Messi na Ronaldinho.

Nafasi ya Pogba kwenye klabu hiyo imekuwa ikizungumziwa kwa muda, na wakala wake Mino Raiola akisema anaona hatima ya mteja wake ni kuwa mbali na Old Trafford.

Maneno hayo yalikuja wakati United walikuwa wakitapatapa katika Ligi Kuu na walikuwa wameondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tangu kupoteza kwa RB Leipzig Desemba mwaka jana, United imeshinda mechi nne na sare michezo miwili kati ya sita ya mwisho kwenye Ligi Kuu na wanalingana kwa alama na Liverpool kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kabla ya mechi ya jana dhidi ya Manchester City.

Pogba amefanya kazi kurudi kwenye kiwango, lakini Ferdinand haogopi ikiwa ataendelea au la.

"Kama akiondoka sioni tatizo, Grealish anaweza kuziba vizuri sana pengo lake," alisema Ferdinand akinukuliwa na Sky Sport.

"Kundoka kwake sio tatizo kwa Manchester. Grealish ana kiwango bora kabisa kama Messi na Ronaldinho."

# Napoli yaikatalia Atletico kwa Milik

**NAPLES,** Italia

KLABU ya Napoli imeikataa ofa ya Atletico Madrid ya kumsajili nyota wake, Arkadiusz Milik, na mshambuliaji huyo pia hataki kwenda Fiorentina.

Napoli wanatajwa kuwa wanahitaji angalau euro milioni 15 ili kumuuza mshambuliaji huyo ambaye kimsingi atakuwa mchezaji huru pale mkataba wake unapoisha Juni 30, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Calciomercato, AS na RMC Sport, Napoli imeikataa ofa hiyo kwa kile kinachotajwa kuwa ni ndogo.

Atletico wanaripotiwa kwamba walikuwa wamejiandaa kutoa kiasi cha euro milioni sita hadi saba kwa nyota huyo raia wa Poland, wakati pia Marseille nao wakiwa hawajajiandaa kufikia dau la euro milioni 15 wanalolitaka Napoli.

Klabu pekee ambayo inaonekana kuwa tayari kutoa ofa ya kiasi ambacho klabu inakitaka ni Fiorentina, lakini mshambuliaji huyu hana mpango wa kuhamia Fiorentina.

Milik amekuwa nje ya kikosi tangu alipokataa kusaini mkataba mpya au kukubali kukamilisha uhamisho.





# RODRIGUEZ AFUNGUKA KUKUBALIKA EVERTON

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Colombia, James Rodriguez, amesema kuwa alichagua kujiunga na Everton kwa sababu alikuwa anahitaji klabu ambayo ingemwamini.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, amekutana tena na kocha wake wa zamani kule Real Madrid, Carlo Ancelotti pale Goodison Park baada ya kutimka Bayern Munich katika muda wake wa mwisho Bernabeu.

Rodriguez alipewa nafasi na Ancelotti na kuwa na mchango mkubwa mwanzoni kabisa mwa msimu.

Baada ya kupata jeraha alilazimika kukosa mechi tano na sasa anaendelea kujitahidi kurejea kwenye kiwango chake.

"Nilitakiwa kwenda kwenye timu ambayo itaniamini. Nilihitaji kucheza chini ya kocha anayenifahamu na tabia yangu ya uwanjani na nje ya uwanja. Nitaishukuru klabu na Carlo wakati wote. Hii ndiyo sababu najitahidi kuonyesha kilicho bora na kucheza kwa bidii katika kila mechi," alisema Rodriguez akinukuliwa na Sky Sport.

Nyota huyo anaamini klabu ya Everton ina njaa ya mafanikio makubwa na yeye ameaminiwa kuwa sehemu ya kutimiza ndoto za klabu hiyo hivyo hana budi kutoa mchango mkubwa haswaa.

# Pochettino awaita nyota wakubwa

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA mpya wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, amesema mchezaji yeyote mkubwa anakaribishwa kuwa sehemu ya familia ya klabu hiyo.

Amesema hayo wakati nyota wa Barcelona, Lionel Messi akiwa anahusishwa kutua ndani ya klabu hiyo.

Pochettino aliulizwa na kuzungumzia pia juu ya ujio wa Messi, Dele Alli na kiungo mshambuliaji Christian Eriksen ambao wamekuwa wakihusishwa na klabu hiyo.

"Kiuhalisia hatujawagusia wachezaji hao, lakini kila mchezaji mkubwa anakaribishwa katika timu yetu," alisema Pochettino ambaye alikuwa anazungumza na waandishi wa habari kwa mara ya kwanza tangu ajiunge na PSG.

Katika dirisha kubwa la usajili lililopita, Messi aliweka wazi matamanio yake ya kuondoka Barcelona ingawa baadaye aliamua kubaki.

Messi amekuwa akihusishwa kwa muda kujiunga na PSG pamoja na Manchester City, lakini Pochettino hajaweka wazi juu ya maingizo mapya, ila inafahamika kuwa Messi anaweza kuwa miongoni mwao.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER AMSHUTUMU KLOPP KUHUSU PENALTI

●●● Huo ndio ukweli, pengine sisi tumepewa nyingi kuliko wao, labda walitakiwa kupewa ...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemshutumu Jurgen Klopp kwa kujaribu kuwashawishi waamuzi kwa kuzungumzia penalti walizopewa Manchester United.

**Klopp anahisi Liverpool ilitakiwa kupewa penalti kwenye mchezo wa Jumatatu ambao walichapwa bao 1-0 na Southampton, huku akilinganisha na penalti nyingi walizopewa United.**

Chini ya Klopp, Liverpool imepewa penalti 46 katika mashindano yote, zikiwamo 30 kwenye Ligi Kuu England.

Na katika muda huo huo chini ya makocha watatu tofauti, United imepewa penalti 67.

Tangu Solskjaer awe kocha mpya wa United Desemba mwaka 2018, United imepewa penalti 42 - huku 27 zikiwa kwenye Ligi Kuu.

Liverpool imepewa penalti 19 tu katika mashindano yote tangu Solskajaer awe kocha wa Man United.

Lakini Solskjaer, ambaye timu yake ilikuwa ikicheza na Manchester City kwenye nusu fainali ya Kombe la EFL jana Jumatano, alionyesha kutoridhishwa na kauli ya Klopp kuhusu penalti.

"Huo ndio ukweli, pengine. Pengine sisi tumepewa penalti nyingi kuliko wao," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini pengine walitakiwa kupewa ... sawa sisi tulipewa... sijui ni penalti ngapi wao wamepewa. Sihesabu penalti ngapi wao wamepewa.

"Hivyo, kama wanataka kutumia muda mwingi kufikiria ni penalti ngapi hawajapewa, mimi huwa sifikirii hilo."

Na Solskjaer anaona kwamba, kauli ya Klopp inajaribu kuwashawishi waamuzi kujadili kuhusu rekodi ya penalti za United.

"Siwezi kuzungumza kwa niaba ya makocha wengine, kwa nini wanasema vitu kama hivi," alisema.

## ZISIKUPITE

### OZIL, DC UNITED WATETA

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, anafanya mazungumzo na DC United kuhusu kuhamia klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Marekani. ***(Football London)***

### RAMOS AKATAA MKATABA

MLINZI wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 34, amekataa ofa ya kuongezewa mkataba wa mwaka mmoja na Real Madrid, ambayo haitaki kwenda kinyume cha sera yao ya kutotoa mkataba wa muda mrefu kwa wachezaji wenye umri kuanzia miaka 30.

### ALABA HUYOOO REAL MADRID

REAL Madrid ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mlinzi wa Bayern Munich raia wa Austria, David Alaba, huku pia Liverpool ikimnyatia nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Guardian)***

### GUARDIOLA NA DE BRUYNE CITY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ana uhakika wa asilimia 100, kiungo wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo, licha ya taarifa kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amepanga kukata ofa hiyo. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL YAMTAKA BUENDIA

ARSENAL imehusishwa na kiungo wa kati wa Norwich, City Emi Buendia, lakini kuna uwezekano mdogo sana wa kumsajili raia huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, kwa sababu ya ukosefu wa fedha. ***(Mirror)***

### KANE, SON HAKIELEWEKI SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imesitisha mazungumzo ya mkataba mpya na nyota wake, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, na Son Heung-min mwenye miaka 28, kutokana na janga la virusi vya corona. ***(Evening Standard)***

### COMAN YUPO SANA BAYERN

WINGA wa Ufaransa, Kingsley Coman amehusishwa na Manchester City na Manchester United, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amesema ana furaha pale Bayern Munich. ***(Bild, via Mirror)***

### PELLE ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham United huenda ikaanza kutafuta mbinu za kumsajili mshambuliaji wa Italia, Graziano Pelle, ambaye ameondoka katika klabu ya Shandong Luneng ya China, kama itashindwa kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth raia wa Norway, Josh King, 28. ***(Star)***

### CEBALLOS KURUDI MADRID

KIUNGO wa Real Madrid, Dani Ceballos, 24, ambaye yuko Arsenal kwa mkopo ana matumaini ya kurejea katika klabu yake hiyo ya utotoni. ***(Cadena Ser, via Evening Standard)***

### KOEMAN ASAKA NYOTA WAPYA

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amesema ametengeneza orodha ya wachezaji "ambao itakuwa bora kama wakipatikana". ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

## Hilika wa Mtibwa anatupia kwao tu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yake ya Mtibwa Sugar kucheza mechi 18 bila yeye kupata bao hata moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, straika wa Mtibwa Sugar, Ibrahim Ahmada Hilika, amefunga bao lake la kwa kwanza akiwa na kikosi hicho cha Manungu, Turiani kwenye Kombe la Mapinduzi, hivyo kuisaidia timu yake kushinda bao 1-0 dhidi ya Chipukizi, kwenye Uwanja wa Amaan, mjini Zanzibar juzi.

Lilikuwa pia ni bao la kwanza la michuano ya Mapinduzi Cup mwaka 2021 na baada ya kufunga bao hilo alionyesha ishara kuwa yeye hufunga zaidi kwenye uwanja huo, au ni kama mfalme wa Uwanja wa Amaan.

Wakati akiwa hajafunga bao kwenye uwanja wowote Tanzania Bara, straika huyo aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu kutoka Zimamoto ya Zanzibar, amewahi kuwa mfungaji bora kwenye Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2016/17 na 2019/20.

## Yanga yampaisha Kipa wa Jamhuri

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuonyesha umahiri mkubwa kwa kudaka na kuokoa michomo ya hatari kutoka kwa wachezaji wa Yanga, kipa wa Jamhuri ya Pemba, Nassir Talib, amesema anaamini uwezo aliouonyesha unaweza kumpa fursa ya kusajiliwa na timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku taarifa zikidai baadhi ya klabu zimeshaanza kummezea mate na kutaka kufanya naye mazungumzo.

Akizungumza baada ya kumalizika mechi ya Kombe la Mapinduzi juzi kati ya timu hiyo na Yanga, Talib alisema pamoja na kwamba ameonyesha uwezo huo mbele ya umati wa watu wengi waliokuja kuhudhuria mechi hiyo, lakini ataonyesha uwezo huo huo hata kwenye mechi zitakazofuata ambazo hazina watu wengi.

"Ni kweli sisi Wanzanzibar tukipata fursa kama hii ya kuonekana na watu wengi, tunaitumia kwa sababu hauonekani sana licha ya kwamba tuna vipaji vya hali ya juu, lakini huu ndio uwezo wangu na hata mechi zitakazofuata nitacheza hivi hivi, na pia nitaongeza juhudi kwa sababu nataka nipate maendeleo mbele ya safari," alisema kipa huyo.

# NAMUNGO NA MKAKATI MZITO KUJIIMARISHA CAF

**Na Saada Akida**

WAKATI wakisikilizia droo ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kujua watapangwa na timu gani mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, uongozi wa Klabu ya Namungo umesema leo unatarajia kupokea ripoti ya Kocha Mkuu, Hemed Morocco, huhusu idadi ya wachezaji anaotaka wasajiliwe katika dirisha hili dogo ili kukiongezea nguvu kikosi hicho.

**Namungo ilirejea jana nchini ikitokea Khartoum, Sudan ambapo juzi iliitoa Al Hilal Obeid kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa jumla ya mabao 5-3 baada ya kutoka sare ya 3-3 matokeo hayo yakija baada ya ushindi wao nyumbani wa mabao 2-0 wiki mbili zilizopita.**

Kwa matokeo hayo, sasa Namungo inasubiri droo ya CAF kujua timu itakayocheza nayo mechi ya mchujo kutoka zilizotolewa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na endapo itaitoa, itatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Selemani, alisema wamefanikiwa kufanya vizuri katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na kusonga mbele, hivyo wanahitaji kuimarisha kikosi chao kwa kusajili wachezaji wa kukiongezea nguvu.

Kuhusu kutajwa kwa mshambuliaji Kwizera Eric kutoka Klabu ya Olympic Star ya Burundi, alisema wanasubiri mapendekezo ya kocha na orodha ya wachezaji anaowataka.

Alisema hana taarifa kuhusu nyota huyo kutakiwa na klabu hiyo, na kwamba dirisha la usajili lilifunguliwa tangu Desemba 15, mwaka jana, lakini hawakuwa na haraka juu ya usajili na leo kabla ya kikosi cha timu kwenda visiwani Zanzibar, watakutana na kocha Morocco kwa ajili ya kupokea majina ya wachezaji anaowataka.

"Tunalipongeza benchi la ufundi na wachezaji wetu kwa kupambana na kufanikiwa kusonga mbele, sasa tunahitaji kuimarisha kikosi chetu kwa kufanya usajili mzuri kulingana na michuano iliyopo mbele yetu," alisema Suleimani.

Alisema hawana mpango wa kumuuza nyota wao yeyote akiwamo Steven Sey anayetajwa kuwamo katika rada za Yanga.

"Hizo taarifa za Sey kutakiwa na Yanga zimekuwa kubwa sana, hatujapokea ofa yoyote na hata kama itakuja hatutakuwa tayari kumwachia mchezaji huyo kwa sababu yupo katika mipango ya benchi la ufundi.

"Hatukubali kumuuza Sey kwa sababu tunahitaji kuimarisha kikosi kwa ajili ya kuendelea kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa pamoja la Ligi Kuu Bara," alisema katibu huyo.

Alisema kikosi kilirejea nchini jana na leo kitaenda visiwani Zanzibar kwa ajili ya kushiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi hii ikiwa ni mara ya kwanza kwao.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa (katikati), akiwatambulisha mabondia Ibrahim Class (kulia) na Shaaban Jongo ambao watapanda ulingoni Januari 29, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Masaki jijini Dar es Salaam kuwania ubingwa wa WBF. Class atawania ubingwa wa Mabara dhidi ya Dennis Mwale anayeishi Afrika Kusini huku Jongo akizipiga na Shawn Miller wa Marekani kuwania ubingwa wa Mabara wa WBF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabondia Class, Jongo kuwania ubingwa wa WBF

**Na Mwandishi Wetu**

MABONDIA wawili wa Tanzania, Ibrahim Class na Shaban Jongo, Januari 29, mwaka huu watapanda ulingoni katika Ukumbi wa Next Door Arena uliopo Masaki jijini Dar es Salaam kuwania ubingwa wa Shirikisho la Ngumi za Kulipwa Duniani (WBF).

Wakati Class atazichapa na Dennis Mwale kutoka Malawi kuwania mkanda wa uzito Superfeather wa Mabara, Jongo ambaye amejizolea umaarufu kwa kumtwanga kwa Knockout (KO) bondia Alphonce Mchumiatumbo, atawania ubingwa wa kimataifa wa WBF wa uzito wa juu dhidi ya bondia kutoka Marekani, Shawn Miller.

Mapambano hayo yamepewa jina la "The Jackson Group Fight Night" ambapo siku hiyo pia kutakuwa na mapambano saba yatakayoshirikisha mabondia wengine wa Tanzania na kutoka nje ya nchi.

Muasisi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema mabondia wote wamekwisha saini mkataba kwa ajili ya kupigana siku hiyo na sasa wapo katika maandalizi makali.

Twissa alisema Class atakuwa anapima uwezo na uzoefu wake katika mchezo wa ngumi za kulipwa kwani Mwale ni bondia mwenye rekodi nzuri na amedhamiria kutwaa mkanda huo.

Class ana rekodi ya kushinda mapambano 24 kupoteza sita wakati Mwale ameshinda mapambano nane na hajapoteza hata pambano moja.

Kwa mujibu wa Twissa, pambano la Jongo na Miller ambalo litakuwa ka raundi 10, pia linatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa kutokana na rekodi za mabondia hao. Jongo ameshinda mapambano saba, kupoteza moja na kutoka sare mawili wakati Mille ameshinda mapambano 18, kupoteza matano na kutoka sare moja.

"Mara ya mwanzo tulizungumzia malengo yetu ya kuendeleza michezo Tanzania na mchezo wa ngumi ndiyo tumeanzia na kupata ushirikiano mkubwa na Shirikisho la Mchezo huo nchini (TPBRC) na WBF huku tukipata sapoti kubwa kutoka kwa Kituo cha Televisheni cha Azam, Global Boxing Stars na Hotel ya Regency Park Hotel. Hii ni ishara kuwa malengo yetu yatafikiwa," alisema Twissa.

Alisema siku hiyo kutakuwa na jumla ya mabondia 18 kutoka nchi tofauti 10 na mabara matatu. "Tunajivunia sana kuvuka mipaka na kuonyesha majukumu yetu katika kuendeleza michezo nchini," alisema.

Michezo
Alhamisi Januari 7, 2021
Nipashe



Solskjaer amshutumu Klopp kuhusu penalti UKURASA 22

HUNIWEZI...



Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akimtoka Perfect Chikwende wa FC Platinum kwenye mechi ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Simba ilishinda 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yamaliza vita Dar

## ●●● Yatinga kibabe hatua ya makundi huku ikilamba bilioni 1.2 za CAF, wachezaji wakoga noti za...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na mabeki, Erasto Nyoni na Shomari Kapombe, na idadi nyingine kama hiyo yakifungwa na straika John Bocco na kiungo mshambuliaji Clatous Chama, yameiwezesha timu ya Simba kushinda 'Vita ya Dar es Salaaam' (War in Dar) dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe kwa ushindi mnono wa mabao 4-0, hivyo kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba, ikiwa na kauli mbiu yake 'War in Dar' kwa kifupi "WIDA", ilikuwa ikihitaji ushindi wa bao zaidi ya moja kupindua matokeo ya kufungwa bao 1-0 wiki mbili zilizopita nchini Zimbabwe dhidi ya wapinzani wao hao.**

Mechi ilianza taratibu na nusura FC Platinum ipate bao dakika ya 20, kama si mkwaju mzuri wa faulo kudakwa kwa ustadi kabisa na kipa Aishi Manula. Shomari Kapombe alivutwa jezi na mmoja wa FC Patinum dakika ya 31 na kusababisha penalti ambayo ililalamikiwa na wachezaji wa timu hiyo, wakitishia pia kutoka nje ya uwanja. Ubishi wao uliendelea kwa dakika sita, hadi walipokubali na Nyoni akaukwamisha wavuni dakika ya 39.

Kapombe, aliwainua vitini mashabiki wa Simba alipoiandikia bao la pili kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Rally Bwalya ambaye alipiga shuti kali lililotemwa na kipa Tizayi kabla ya kumkuta mfungaji, akaukwamisha wavuni.

Platinum ilikuja juu, lakini wakati wakisukuma mashambulizi mbele, wachezaji wa Simba walirudi nyuma na kuzuia zaidi, ikifanya mashambulizi kwa kushtukiza. Hiyo iliisaidia Simba kwani dakika ya kwanza ya nyongeza, Bocco aliifunga bao la tatu, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Chama aliyekokota mpira umbali mrefu na kuingia nao, akampasia Bwalya aliyeonekana kama yeye ndiye atapiga golini lakini akampasia mfungaji ambaye aliingia kuchukua nafasi ya Meddie Kagere aliyeumia muda mchache tu baada ya kuingia kuchukua nafasi ya Chris Mugalu.

Chama tena alikokota mpira na kuingia ndani ya eneo la hatari, kabla ya kuangushwa chini, mwamuzi akaamuru penalti na yeye mwenyewe akaukwamisha wavuni.

Kwa matokeo hayo Simba inaingia kwa mara ya tatu kwenye hatua ya makundi, huku ikiingia mara ya pili baada ya miaka miwili, kwani 2018 ilitinga hatua hiyo. Aidha, kwa kuingia hatua ya makundi tayari inajihakikishia kuvuna Sh. bilioni 1.2 kutoka Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF). Lakini wachezaji wa timu hiyo watakuwa wamejinyakulia kitita Sh. milioni 250 walizoahidiwa na Mwekezaji wa timu hiyo Mohamed "Mo" Dewji kwa ushindi huo.

Simba sasa inasubiri makundi kupangwa Januari 17 na mechi ya kwanza ikitarajiwa kupigwa Februari 6, mwaka huu, huku FC Platinum sasa ikisubiri kupangwa na timu moja kutoka Kombe la Shirikisho na kama ikipata matokeo ya jumla itacheza hatua ya makundi ya kombe hilo la pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

### TAHARUKI

Simba walianza kuingia uwanjani na kupimwa joto baada ya hapo waliingia moja kwa moja katika vyumba vya kubadilishia nguo, taharuki ilitokea baada ya kuingia wachezaji na viongozi wa benchi la ufundi la Platinum nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, badala ya kushuka kupitia mlango wa basi, wakatokea kwenye vioo.

# Yanga sasa hasira kwa Namungo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikihenyeshwa na kulazimishwa sare tasa kwenye Kombe la Mapinduzi dhidi ya timu ya Daraja la Kwanza Zanzibar, Jamhuri ya Kisiwani Pemba, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, ametoa sababu ya matokeo hayo huku akisema hatafanya makosa katika mechi ijayo.

Yanga ambayo juzi ilishindwa kufurukuta dhidi ya vijana hao wa Pemba, kesho itashuka tena katika Uwanja wa Amaan kuvaana na Namungo FC iliyotoka kuwatoa Al Hilal Obeid ya Sudan kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Namungo imesonga mbele kwa jumla ya mabao 5-3 baada ya juzi kutoka sare ya 3-3, ikiwa ni baada ya mechi ya awali nyumbani katika Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam kushinda 2-0.

Akizungumza na Nipashe uwanjani hapo baada ya sare hiyo, Kaze alisema matokeo hayo yametokana na wachezaji wake kuchoka kutokana na michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo ana uhakika wa kufanya vizuri katika mechi ijayo, kesho dhidi ya Namungo.

"Wachezaji walitumika sana katika michezo ya Ligi Kuu hususan ile ya mikoani ambayo walilazimika kusafiri umbali mrefu, walihitaji kupata mapumziko zaidi, hata hivyo nawapongeza kwa kucheza vizuri," alisema kocha huyo raia wa Burundi huku akifafanua kuwa kupitia mchezo huu kipo kitu kipya ambacho wamekipata.

Kwa upande wa Kocha wa timu ya Jamhuri, Mfaume Shabaani, alisema wanaiheshimu Yanga kwa kuwa ni timu yenye uzoefu katika mashindano mbalimbali, hivyo wachezaji wake wanastahili pongezi kwa kiwango walichokionyesha.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042